Jumanne Agosti 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581774
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 22

**ANCELOTTI AKOSOA KIWANGO CHA MADRID**

**Janabi** ataja sababu watu wanaoshindwa kufunga mlo

UKURASA 4



**Hali** ya hewa yakwamisha mapokezi ya ndege mpya

UKURASA 5

**ACT** yalalamika upandishwaji kinyemela wa kodi ya majengo

UKURASA 17

# Sakata binti aliyebakwa sasa lachukua sura mpya

• **Kamanda** aliyedai alijiuza atumbuliwa, watuhumiwa wapandishwa kizimbani kwa siri... *Endelea Ukurasa 3*



**Je, Watuhumiwa ni maofisa wa jeshi lipi?... Binti alilazimishwa kumwomba msamaha 'Afande'. Je Afande ni nani?" –**

Dk. Anna Henga



**"Licha ya nchi kuwa na viongozi wakuu wanawake, haki ya binti huyo inachelewa kupatikana" –**

Boniface Jacob



Watuhumiwa wa ubakaji (kulia mwenye fulana nyekundu na madoa) wakiwa chini ya ulinzi wakisubiri kusomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma jana.

UKURASA WA 7

## HOSPITALI ZASISITIZWA GHARAMA STAHIMILIVU

WADAU wa sekta binafsi wanaojihusisha na utoaji wa bima ya afya nchini wametoa wito kwa hospitali mbalimbali nchini kuacha kuweka gharama kubwa za matibabu badala yake waweke viwango ambavyo vitakuwa stahimilivu kwa Watanzania wa hali zote...

## Waziri aomba benki kuunga mkono CRDB kukopesha wachimbaji


UKURASA 8

## MOI yakiri ongezeko tatizo nyonga, magoti

UK. 2

**MICHEZO** GAMONDI ATAKA YANGA KUFUZU KWA REKODI CAF UK.24

**MAONI,** UK.6




Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (wapili kulia) akikabidhi mfano wa hundi ya Sh.Bilioni 10 kutoka benki ya CRDB ili kuwainua wachimbaji wadogo nchini. Wapili kushoto ni Ofisa Biashara Mkuu wa benki hiyo, Boma Raballa. Habari uk.8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MOI yakiri ongezeko tatizo nyonga, magoti

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oxford cha Uingereza, imefanya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 20, wakiwamo wanne wa marudio.

Wakati hayo yakifanyika, taasisi hiyo imesema kuna ongezeko la tatizo na mahitaji ya upasuaji huo nchini na kwamba hadi sasa wagonjwa 12,000 wameshapatiwa huduma hiyo upasuaji na wengi wanaougua ni kuanzia miaka 50 na kuendelea.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Lemeri Mchome, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati taasisi hiyo ikiadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake ikiweka kambi ya siku nne iliyoanza jana, kwa kuwafanyia upasuaji huo wagonjwa hao.

Alisema kambi hiyo inafanywa na MOI kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Oxford na wengine kutoka Australia, ili kufanikisha upasuaji huo.

Kuhusu miaka 20 ya taasisi hiyo, Dk. Mchome alisema wagonjwa wengi ambao wanafanya upasuaji wa kurudia, wengi wao wana matatizo katika mifupa kwa kuwa na uvimbe unaohitaji huduma ya aina hiyo, ambao awali walitibiwa nje ya nchi.

"Tuna uwezo wa vifaa na miundombinu kwa kufanya upasuaji huu. Hii ni kutokan ana uwekezaji wa serikali. Tangu tumeanza kufanya upasuaji ni wagonjwa zaidi ya 5,000 ambao tumewatibu kwa kuwabadilishia nyonga na magoti.

"Upasuaji wa magoti pekee ni wagonjwa wengi zaidi wapatao 8,000 wana matatizo mbalimbali ambayo hayahitaji kubadilishwa lakini wanahitaji tiba mbadala," alisema Dk. Mchome.

Aliongeza kwamba tatizo ni kubwa na kwa uzoefu katika takwimu zinaonesha bado kuna wagonjwa wengi wa kubadilisha nyonga na magoti takribani 200 wanaosubiri huduma.

"Arusha pekee katika kambi, tulipata wagonjwa 104 ambao tayari wanasubiria upasuaji wa nyonga na magoti. Bado tuna zaidi ya wagonjwa 50 katika foleni ya kusubiri upasuaji wa kurudia wa nyonga na magoti," alibainisha Dk. Mchome.

Bingwa Mbobezi katika Upasuaji wa Mifupa na Uti wa Mgongo na Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa Mifupa MOI, Dk. Anthony Assey, alisema kwa miaka 20 taasisi hiyo inafurahia mafanikio ya upasuaji wa aina hiyo ambao ni wa kibingwa.

Alisema pia huduma kama hiyo, imefikishwa na taasisi hiyo katika hopitali tofauti nchini ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Hospitali ya Tiafa Muhimbili (MNH)-Mloganzila na Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na Mnazi Mmoja ya Zanzibar na zingine za kanda.

"Miaka 20 hii ni ya kazi kubwa na kambi inayoanza leo (jana) kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Oxford kutoka Uingereza kwa ufadhili wa kampuni ya Signature kutoka Australia, tunatarajia kufanya upasuaji wa marudio kwa wagonjwa wanane na wengine 12 upasuaji wa mara ya kwanza.

"Matatzio haya ya magoti ni ambayo yapo sana na takwimu inaonesha, watu waliofikisha zaidi ya miaka 50 matatizo huanza na unapofikisha umri wa zaidi ya miaka 60 kwa asilimia 50 watakuwa na maumivu ya aina fulani ya magoti na nyonga.

"Na umri unapokwenda zaidi ndipo upasuaji unapohitajika, na ukishafanyiwa unahitajika kufanyiwa marudio baada ya miaka 15, ili kubadilisha kifaa baada ya kuwa katika uchakavu," alisema.

Naye Bingwa Mbobezi wa Nyonga na Misuli kutoka Houston, Texas nchini Marekani, Dk. William Stocks, alisema kupitia taaisi anayofanyia kazi, alibaini kwa nchi zinazoendelea ni kikwazo kwa watu wake kupata huduma aina hiyo, kutokana na gharama za upasuaji zinazofikia zaidi ya dola 2,000 za kimarekani.

"Taasisi yetu ikaamua kushirikiana na MOI kutoa huduma hiyo kwa nchi za eneo hilo, ikiwa ni mpango wa kiutu, tunatarajia kufanya huduma hiyo kwa Watanzania wengi ambao wana tatizo," alisema Dk. Stocks.

hosplan
hitech Sai HOSPITAL
sarvodaya HEALTHCARE

Eminent specialist Doctors from Sarvodaya Hospitals, Delhi, India

Free
Medical Camp
TERMS & CONDITION APPLY
FOR 10 FIRST PATIENTS
Special consultations for Back pain
All Spine, Brain and Back ache issues
All Knee, Hip joints and bones issues

Venue: Hi-Tech Sai Hospital, Upanga, Dar Es Salaam.
Dates: 22,23,24 August

Dr Yawar Shoaib Ali
Neurosurgeon (Brain and Spine)

Dr Anchit Uppal
Orthopedic surgeon ( Bone and Joints)

Send us a WhatsApp message on +255 761460999 or email on amit@hosplan.com to book your appointment today!







# Serikali yatoa kauli maandamano Ngorongoro

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu madai yaliyotolewa na baadhi ya wananchi wa Ngororo kuwa wanakosa huduma muhimu.

Kaimu Meneja wa Uhusiano kwa Umma wa NCAA, Hamis Dambaya, aliiambia Nipashe jana na kufafanua kuwa, madai ya wananchi hao kwamba hawana huduma nzuri za kijamii si ya kweli kwa kuwa wanapata huduma zote muhimu kama ilivyo kwa Watanzania wengine.

"Huduma zote za msingi wanapata, wanapewa na serikali kama wananchi wengine, kuna shule, vijiji kuna hospitali kila kitu kipo," alisema Dambaya.

Taarifa aliyotoa kwa umma baadaye ilisema licha ya kuwapo kwa maandamano hayo, shughuli za utalii zinaendelea vizuri na kuwa wanawahakikishia usalama watalii kutoka ndani na nje ya nchi wanaoendela safari zao.

Alisema uwapo wa maandamano hayo unaidhihirishia dunia, jumuiya ya kimataifa, vyombo vya habari na asasi za kimataifa kwamba ndani ya hifadhi hiyo hakuna ukiukwaji wa haki za binadamu na unyanyasaji wa wananchi.

"Mamlaka inawahakikishia watalii wote waliopanga safari za kuja Ngorongoro kuwa serikali itaendelea kusimamia usalama wao wakati wote watakapokuwa ndani ya hifadhi.

"Watalii kutoka ndani na nje ya nchi wameendelea na safari zao za kushuhudia vivutio vya utalii ndani ya hifadhi na serikali inaendelea kuwahakikishia usalama wao," alisema.

Waandamanaji hao walidai kuwa, wanataka haki ya kurudishwa kwenye orodha ya wapigakura ili washiriki uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba, mwaka huu, na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Video mbalimbali zilizorushwa kwenye mitandao ya kijamii zilionesha kundi hilo likiwa limeziba barabara hiyo huku likiimba nyimbo na kulazimisha misafara ya magari yaliyobeba watalii kusimama kwa muda.

Kupitia video hizo, jamii hiyo ilieleza kuwa wamelazimika kufikia uamuzi wa kuandamana kwa amani jana asubuhi kudai serikali iwarejeshee haki zao za msingi ambazo zilizopuuzwa kwa miaka mitatu, kubwa likiwa ni kuondolewa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura, huku wakiendelea kulipa kodi kama Watanzania wengine.

Mmoja wa wanajamii, Ezekiel Olemangi, alisema wamefuatilia haki yao ya kupiga kura kwenye taasisi husuka ikiwamo Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) bila mafanikio yoyote.

"Lakini hivi karibuni lililoleta shida zaidi ni sisi kuondolewa kwenye orodha ya wapiga kura wa nchi hii, kimsingi tumejaribu kupiga kelele na kufuatilia kwenye taasisi zinazohusika ikiwamo kwenye Tume ya Uchaguzi na TAMISEMI, lakini kila mmoja anarusha mpira kwa mwenzake," alisema.

Pia, alisema licha ya kuendelea kulipa kodi kama Watanzania wengine kwa miaka mitatu, hadi sasa hakuna mradi wowote wa kuchochea maendeleo umefanyika katika eneo hilo, huku kukiwa na vitisho vingi vyenye kukatisha tamaa ikiwamo askari wa mamlaka hiyo kufanya doria kwenye maboma ya wanakijiji.

Aidha, alisema walifanya juhudi mbalimbali za kuomba kukutana na kuzungumza na mamlaka husika kama vile kuandika barua kwa viongozi wa juu, kuomba kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan mara kwa mara bila mafanikio yoyote hivyo wanaona kuwa, njia pekee iliyobaki ni kufanya maandamano ya amani kwa kuwa hawana sehemu yoyote ya kuishi zaidi ya ndani ya eneo hilo.

HABARI KITAIFA

# Sakata binti aliyebakwa lachukua sura mpya

**Na Jenifer Gilla**

SAKATA la binti anayedaiwa kuwa mkazi wa Yombo Dovya, Temeke mkoani Dar es Salaam, aliyebakwa na kulawitiwa na wanaodaiwa kuwa askari walitumwa na bosi wao 'Afande', limechukua sura mpya.

Hatua hiyo ni baada ya mjadala mkali kuibuka katika mitandao ya kijamii kutokana na kauli iliyotolewa juzi na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Theopista Mallya, alipohojiwa na gazeti la Mwananchi na kusema uchunguzi wa jeshi hilo umebaini kuwa binti huyo alikuwa anajiuza.

Hata hivyo, saa tano baada ya habari hiyo kusambaa, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alitangaza kumhamishia Kanamda Malya makao makuu ya jeshi hilo.

Alisema pia jeshi hilo lilibaini vijana wanaotuhumiwa kumfanyia binti huyo kitendo hicho walikiri kutoagizwa na askari kama ilivyoelezwa na pia walikuwa walevi na wavuta bangi.

Baada ya taarifa hiyo kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii iliibua hisia kali kwa wananchi ambao waliandika ujumbe wa kulilaumu jeshi hilo kwa kutomtendea haki binti huyo huku wakiamwambatanishia Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, wakiwataka waingilie kati.

Meya wa zamani wa Ubungo, Boniface Jacob, ambaye aliibua sakata hilo wiki mbili zilizopita, aliandika maelezo yenye ukurasa wake wa X akieleza masikitiko yake kuwa licha ya nchi kuwa na viongozi wakuu wanawake, haki ya binti huyo inachelewa kupatikana.

Alisema inasikitisha licha ya Kamanda wa Polisi Dodoma ambaye ni mama, kushiriki kuhukumu na kuharibu kesi ya mwanamke mwenzake kwa kusema maneno mabaya na ya uongo hadharani, ili binti akose msaada na kupoteza haki yake.

Jacob alisema binti huyo hakuwa anajiuza kama alivyosema kamanda bali anafahamika kwa mwenendo mzuri, aliyepaswa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu kama si kukatisha masomo yake akiwa kidato cha pili baada ya kushindwa kuelewa masomo darasani na kuajiriwa kufanya kazi katika baa iliyoko Dodoma.

Alisema kauli hiyo, iliyokanushwa na jeshi hilo kuwa si ya taasisi, kwamba alikuwa anajiuza ilhali amefanyiwa kitendo cha kinyama, inamuumiza zaidi binti huyo na familia yake na kutafsiri kama nia ovu ya kupoteza haki yake.

"Ninatarajia kuona katika kesi hii wanawake wote Tanzania wanaungana kumtetea binti JM na kujakikisha haki inatendeka kama sehemu ya kulinda wanawake wengine dhidi ya ubakaji na udhalilishaji," aliandika Jacob.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa alitegemea kuona kauli za polisi zikiwa zimejaa utu, haki na huruma kwa binti huyo kwani hata angekuwa kweli anajiuza hakustahili kufanyiwa vitendo hivyo vya ukatili.

"Mtoto wako angefanyiwa ukatili huu na video zake kusambazwa pengine kauli zenu zingejaa utu, haki na huruma , mtalipa kila dhambi mnayoitunza kwa maelezo," alisema.

Mmoja wa watumiaji wa mitandao hiyo, Carol Ndosi, aliandika kwenye ukurasa wake wa X kuwa kitendo alichofanyiwa binti huyo ni cha kinyama na wale wote wanaotengeneza mazingira ili waliohusika wasiwajibishwe ni wanyama zaidi.

Mtumiaji mwingine aliyejulikana kwa jina la Choki Junior, alihoji kwenye ukurasa wa Instagram kuwa: "Hata awe anajiuza ni haki afanyiwe vile? Ukiangalia tu video unahisi aliridhia kufanyiwa vile kwa sababu ya pesa? Mvuta Bangi au mlevi yuko sahihi kumtendea mtu vile? Vaa viatu vya mzazi wa yule binti halafu polisi unaowategemea wanakuletea taarifa hivi, kichaa anachekesha sana kama hatoki kwenye familia yako."

**WAZIRI AINGILIA KATI**

Kauli hizo zilimwibua Waziri Gwajima na kuandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa amepokea hisia, maoni na maswali ya wananchi na amewasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni na anayafanyia kazi.

"... ni dhahiri kuwa alichofanyiwa 'Binti wa Yombo' ni kitu kibaya kisicho cha utu hivyo, anastahili haki yake kwa mapana yote. Ndugu Wananchi, Nawasihi tujipe muda na kuamini kuwa, haki itatendeka kwa mujibu wa sheria na itaonekana bayana na siyo vinginevyo," aliandika Waziri Gwajima.

**POLISI YAOMBA RADHI**

Baada ya taarifa hiyo kusambaa, polisi waliibuka na kutoa taarifa ya kuomba radhi kwa Watanzania na kumhamisha Kamanda Theodora kituo cha kazi wakati uchunguzi wa usahihi wa kauli aliyoitoa ukiendelea.

Taarifa iliyotolewa Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu kamishna (DCP) David Misime, jana ilisema kauli iliyotolewa si ya jeshi hilo bali ya mtu binafsi na kuwa kauli sahihi ni zile alizozitoa kwa umma Agosti 4,6 na 9, mwaka huu, na watuhumiwa walifikishwa mahakamani jana.

"Jeshi la Polisi lingependa kuomba radhi kwa kila mmoja aliyeguswa na kuchukizwa na kauli hiyo inayosambaa kwenye vyombo vya habari wakati ufuatiliaji ukifanyika kupata usahihi wake.

"Wakati uchunguzi wa kupata usahihi wa kauli hizo ukiendelea, Mkuu wa Jeshi la Polisi amefanya mabadiliko madogo kwa kumhamisha Kamanda Theopista Mallya kwenda Makao Makuu ya Polisi Dodoma na nafasi yake kuchukuliwa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi," alisema Misime.

**WABUNGE WANAWAKE**

Nao wabunge wanawake wamelipongeza Jeshi la Polisi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hatua za awali za kumwondoa Kamanda Mallya.

"Tunataka haki itendeke kwa binti aliyebakwa na kulawitiwa na wahusika wote wafikishwe mahakamani haraka akiwamo anayetuhumiwa kuwatuma kubaka na kulawiti," lilisema tamko hilo.

**LHRC YAIBUKA**

Jana Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kilitoa taarifa kwa umma kuwa kuna maswali 11 kwenye taarifa zinazotolewa na polisi.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, aliuliza maswali hayo kuwa ni taarifa zipi ni sahihi kutoka Jeshi la Polisi Makao Makuu, Wizara Mambo ya Ndani au Makamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam na Dodoma? Je, Watuhumiwa ni Maafisa wa Jeshi lipi?

Maswali mengine watuhumiwa katika tukio hilo walikuwa watano, je huyo mwingine ni nani na yuko wapi? binti alilazimishwa kumuomba msamaha 'Afande', je Afande ni nani? Je Mhanga yuko salama katika mikono ya wanaomhumkumu kuwa ni kama alikuwa anajiuza?"

Je, Binti huyo kuwa katika mikono ya Polisi hakutaathiri upatikanaji wa haki na ushahidi?, Je Mtu kuwa kama anajiuza inahalalisha kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwepo kubakwa?, Je kwa vitendo hivi Jeshi la Polisi linasimamia maslahi ya nani?"

Je kuwa mlevi na mvuta bangi ni kinga dhidi ya uhalifu?, Kwa kutajwa Afande bila kusema ni Afande wa Jeshi gani je Polisi hawana mgogoro wa maslahi na hili shauri? Na taarifa ya Polisi ya August 9 2024 ilisema upelelezi umekamilika na leo ni tarehe 19, je ni lini shauri hili litapelekwa Mahakamani?"

"LHRC inapenda kuwakumbusha kuwa kitendo alichofanyiwa muhanga ni cha kinyama, kikatili, kinyume na haki za binadamu na sheria za Nchi na kwamba yeyote atakayefumbia macho vitendo hivyo ni adui wa haki na utu, LHRC inapenda kutoa wito kwa Jeshi la Polisi kuacha kulinda na kutetea uhalifu kwani kauli ya RPC Dodoma ni wazi inatetea wahalifu na uhalifu uliofanyika," alisema Henga.

"Pia Polisi itoe nafasi kwa Binti Muhusika kupata huduma ikiwepo ya ushauri nasihi kutoka kwa chombo ambacho hakina maslahi na shauri hili," aliongeza.

# ...Watuhumiwa ubakaji, ulawiti wafikishwa mahakamani

**Renatha Msungu na Paul Mabeja, DODOMA**

WATU wanne wanaotuhumiwa kutumwa na askari kumlawiti na kumbaka binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Saalam, jana walifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma na kusomewa mashtaka mawili.

Watuhumiwa hao walifikishwa mchana katika mahakama hiyo na kusomewa mashtaka ya kubaka kwa kikundi (gang rape) na kumwingilia kinyume na maumbile binti huyo.

Washtakiwa hao wametajwa kuwa ni Clinton Damas, Askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Amin Lema, Nickson Jackson na Praygod Mushi ambaye ni Askari wa Jeshi la Magereza.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani wakiwa chini ya ulinzi wa polisi, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Zabibu Mpangule.

Ilidaiwa mahakamani hapo ya kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Mei 25 na Mei 26, mwaka huu.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikana mashtaka na kesi hiyo imepangwa kuanza kusikilizwa leo mchana.

Akizungumza nje ya mahakama Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu, Renatus Mkude, alisema kuwa mahakama imetoa amri ya kumlinda binti aliyefanyiwa ukatili kwa jina lake kufichwa ili asipate fedheha na kudhalilika.

"Na washtakiwa wamenyimwa dhamana kwa sababu za kiusalama na wataendelea kubaki rumande," alisema.

Alisema kuwa kesi hiyo ambayo upelelezi wake umekamilika itaanza kusikilizwa mfululizo kuanzia leo hadi Ijumaa wiki hii.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuwa na utulivu wakati sheria inachukua mkondo wake.

"Tunaamini haki itatendeka kadiri sheria inavyotaka, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka itahakikisha haki inatendeka," alisema.

Katika hali ambayo haikutarajiwa waandishi wa habari walizuiwa kuingia kwenye chumba maalum ambacho watuhumiwa hao walifikishwa mbele ya hakimu, na kulazimika kupata maelezo ya kesi kwa wanasheria na hakimu.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu (wapili kushoto) akipokea maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi House Investments, Dk Fred Msemwa kuhusu mradi wa Watumishi House unaotekelezwa na WHI katika eneo la Magomeni Usalama, Dar es Salaam jana. Sangu alitembelea WHI na kukagua maendeleo ya mradi huo wa nyumba za watumishi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa WHI, Sephania Solomon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Janabi ataja sababu wanaoshindwa kufunga mlo

**Na Christina Mwakangale**

TOFAUTI za miili kati ya mtu mmoja na mwingine, ni moja ya sababu zisizoweza kuwalinganisha hasa inapotokea suala la kufunga kula huku mwingine akistahimili na mwingine kushindwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, anasema miili inatofautiana namna inavyofanya kazi kutokana na namna ilivyoundwa (jenetiki).

Bingwa huyo katika magonjwa ya moyo, anafafanua hayo katika kitabu chake 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako, akieleza sababu sita kwa nini wengine wanashindwa kufunga.

Anasema tofauti hizo za miili pia na mazingira mtu anapoishi, hali ya hewa, aina ya kazi unayofanya na aina ya chakula na mapokeo yake katika mwili ni sababu za wengine kushindwa kufunga.

"Matokeo ya afua kama za kufunga yatakuwa tofauti hata kama watu wawili watafanya afua moja kwa usahihi wa asilimia mia moja. Kuna watu ambao huchakata hifadhi ya chakula kwa haraka na wale wanaochakata taratibu.

"Ni vyema kujifunza mwili wako ni wa aina gani na ni matokeo gani ungeyataka. Wako watu wanaojaribu kufunga lakini kutokana na sababu mbalimbali zinazotokana na utaratibu wa ufungaji, hujikuta wakishindwa kuendelea kufunga, hivyo huacha," alisema bingwa huyo wa tiba ya moyo.

Alitaja sababu zingine za kushindwa kufunga kuwa ni pamoja na kupungua uzito kupita kiasi. Anasema wako wanaopoteza uzito kwa kiasi kikubwa, hivyo huona kuwa hayakuwa malengo yao kuwa wembamba hivyo.

"Kwa hiyo wanakuwa na wasiwasi, wanaacha kuendelea na utaratibu wa kufunga. Hawa pia huenda ni kundi lile la wale wanaochakata mfumo wa chakula kwa haraka.

"Yaani kwa jitihada ndogo wanaweza kupungua kwa kasi sana. Pia ikumbukwe kuwa kupungua uzito kuliko inavyotakiwa kunasababisha utapiamlo ambao nao ni ugonjwa," anasema.

Prof. Janabi anataja sababu nyingine ya watu wengine kushindwa kufunga kuwa ni kutopungua uzito. Anasema kwa watu ambao matarajio yao hayafikiwi, kwa maana ya muda ambao walidhani wangekuwa wamepunguza uzito wa mwili, lakini matokeo yanakuwa kinyume chake.

"Mara nyingi kundi hili ni la wale ambao wako kwenye shinikizo la makundi kama kwenye mitandao ya jamii kwamba kuna uwezekano wa kupunguza uzito ndani ya muda mfupi. Sasa wanapoona kwamba matarajio yao hayakufikiwa, wanakata tamaa na kuacha kuendelea kufunga," anaongeza.

Sababu nyingine, kwa mujibu wa Prof. Janabi, ni uzito kupungua kwa taratibu mno. Anasema wako watu ambao matokeo ya kupungua uzito hutokea taratibu sana.

"Hali hiyo huwakatisha tamaa kwa kuwa walitarajia matokeo ya haraka ya kupunguza uzito. Wanapoona hali hiyo, hupoteza uvumilivu na hivyo kuachana na utaratibu wa kufunga. Aina hii huenda ni wale wanaochakata taratibu na wanahitaji muda na jitihada zaidi kufikia lengo," anabainisha.

Prof. Janabi pia anasema kupanda na kushuka kwa uzito ni sababu za baadhi kushindwa kufunga, wakiwamo watu ambao kutokana na kufunga, wanapata hali mchanganyiko ya kupungua na kuongezeka uzito.

"Hali hii inawakatisha tamaa kwa sababu wanaona malengo yao ya kufunga hayafikiwi, hivyo huamua kuacha kuendelea na utaratibu wa kufunga.

"Kama nilivyosema awali, mwili unayo namna ya kujisahihisha. Afua ya kufunga ikizoeleka, mwili unaweza kutafuta namna ya kujilinda na kujirejesha katika hali iliyojizoesha ndio maana kufunga kwa vipindi na sio moja kwa moja ni muhimu zaidi kama afua ya afya," anasema na kuongeza kuwa mwili pia unaweza kushindwa kuhimili madhara ya kufunga.

"Binadamu wanatofautiana jinsi miili yao inavyopokea hali ya kufunga. Wapo wanaopata madhara kama ya kuumwa tumbo, kutapika, au kuumwa kichwa na mengine.

Kutokana na hali hii, kufunga kwao kunageuka kuwa kero na kuwaharibia utulivu wa maisha na afya zao. Hawa nao huamua kuachana na utaratibu wa kufunga. Pia anasema watu hao hushindwa kuhimili njaa kali, akisema hiyo ni dhahiri kufunga kula huambatana na njaa na hisia za zinapokuja mwili unatoa ishara ya kutaka chakula.

"Sasa wako watu ambao hawahimili kukaa na njaa au kuwa na njaa kali sana kiasi cha kuwafanya washindwe kuivumilia. Matokeo yake huona kuendelea kufunga ni kama adhabu ambayo haina maana kwao. Hivyo, watu hawa huacha kufunga na kuendelea na utaratibu wa kawaida," anasema.

Prof. Janabi aanasema wataalamu wanapozungumza kuhusu ulaji bora wenye afya, haimaanishi kukataza watu kula.

"Tunasema katika utaratibu wa ulaji wako ndio unasababisha kuwa na kiwango cha juu au cha chini cha insulini mvwilini. Kama ambavyo tumeona, ongezeko insulin ndiyo kichocheo cha kuongezeka kwa uzito wa mwili. Katika utaratibu wa ulaji wa chakula tunapaswa kujua vitu muhimu.

"Unakula mara ngapi kwa siku; Unakula mchanganyiko gani wa chakula?; Unakula saa ngapi na kiasi gani?; Unakula muunganiko na mgawanyiko wa aina gani ya chakula kama wanga, protini, au mafuta," anasema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa tatu unaanza kufanyika tarehe 21 hadi 27, Agosti, 2024 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 21 na kuhitimishwa Jumanne tarehe 27 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 16 Agosti, 2024 na:**

**Kalima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**



Kamal

**KAMAL REFINERY LIMITED**

# TAARIFA KWA UMMA

**Kamal Refinery Limited,** Kiwanda pekee cha kuchakata oil chafu Tanzania kilichopo Kerege, Bagamoyo.

Tunapenda kuutangazia umma kwamba tunanunua mafuta yaliyotumika ya injini (kutoka kwa meli, boti, pikipiki, magari, mabasi, malori na vifaa vya kilimo na madini, vifaa vya ujenzi), mafuta ya gia yaliyotumika, na vilainishi vya viwandani vilivyotumika kwa lengo la kuyachakata tena ili yaweze kutumika kwa matumizi mengine. Hivyo, tunapokea maombi kutoka mikoa yote Tanzania kwa wauzaji wa mafuta chafu na wale wenye nia ya kuanza kufanya biashara hii.

Tunawaalika wauzaji wa mafuta machakavu kutoka maeneo yote ya Tanzania, pamoja na wale wanaopenda kuanza biashara hii, kuchukua hatua ya kuwasiliana nasi.

Kama unauza mafuta machakavu sasa au unapanga kuanza, hii ni fursa muhimu. Tafadhali wasiliana nasi kwa simu nambari **0768 690 137 au 0767 202122.**

Kufanya kazi nasi sio tu kufanya biashara, bali pia inachangia katika kulinda mazingira. Oil yako yatashughulikiwa kwa uwajibikaji, kuhakikisha hayatumiki vibaya, jambo ambalo husaidia kuepuka madhara yanayosababishwa na matumizi mbaya ya oil chafu.

HABARI KITAIFA

# Mpango ataka eneo kilimo cha zabibu lilindwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Dodoma kuhakikisha ardhi inayotengwa kwa ajili ya kilimo cha zabibu inalindwa isivamiwe kwa ujenzi wa makazi.

Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jana, baada ya kuweka jiwe la msingi la Kiwanda cha Kusindika Zabibu kilichopo Chinangali II Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, akiwa katika siku ya kwanza ya ziara ya kikazi mkoani humo.

Alisema kasi ya ujenzi wa makazi imekuwa kubwa mkoani Dodoma, hivyo ni vyema wataalamu wa mipango miji na wapimaji viwanja kuzingatia maeneo ya kilimo cha zabibu kubaki kama yalivyopangwa.

Pia aliwataka wananchi wa mkoa wa Dodoma kuongeza jitihada katika kulima zabibu, ili kiwanda hicho kiwe na manufaa zaidi.

Alisema Tanzania hutumia takriban Sh. bilioni 19.5 kila mwaka kuagiza wastani wa lita milioni 10 za mchuzi wa zabibu nje ya nchi, ili kukidhi mahitaji ya ndani

Uwapo wa kiwanda hicho, alisema utatatua changamoto nyingi za usindikaji na uhifadhi wa zabibu pamoja na kuzuia upotevu kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya kuongezea thamani na uhifadhi.

Aliongeza kwamba viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ikiwemo zabibu kwa ajili ya matumizi yetu ya ndani na kuuza ziada nje ya nchi ni miongoni mwa vipaumbele muhimu katika ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Makamu wa Rais alisema serikali imeliingiza zao la zabibu katika orodha ya mazao ya kimkakati ambayo ni ya kipaumbele katika kuendelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Aidha, alimwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuhakikisha upatikanaji wa miche bora kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), na halmashauri za wilaya husika, pamoja na kuimarisha huduma za ugani za zao la zabibu.

Dk. Mpango alitoa wito kwa wananchi wa Dodoma kuepukana na uharibifu wa mazingira ikiwemo uchomaji moto na kukata miti ovyo.

Aliwataka kuzingatia wajibu wa kutunza vyanzo vya maji na ardhi oevu, ili kuunusuru mkoa huo na athari za mabadiliko ya tabianchi.



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, akizungumza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari alipomtembelea ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma jana kwa lengo la kujitambulisha kwake baada ya kuapishwa na Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hali ya hewa yakwamisha mapokezi ndege mpya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MABADILIKO ya hali ya hewa yamesababisha kusitishwa kwa mapokezi ya ndege mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner iliyotarajiwa kutoka nchini Marekani kupokewa Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar, jana.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alitarajiwa kuzindua ndege hiyo pamoja na viongozi mbalimbali wa kitaifa na wananchi.

Ndege hiyo inamilikiwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na ina uwezo wa kubeba abiria 262, viti 22 vya daraja la biashara na 240 ni daraja la kawaida, pia ina uwezo wa kubeba mizigo kati ya tani 15 hadi 20 kulingana na ujazo wa abiria na mizigo.

Maandalizi ya hafla hiyo yalikamilika na wananchi waliofika katika eneo la tukio walirejeshwa kutokana na kughairishwa kwa hafla hiyo.

Mapema asubuhi askari wa vikosi vya ulinzi vya SMZ waliwekwa katika lango kuu la kuingi kwenye viwanja hivyo na kuwarejesha wananchi na viongozi mbalimbali ambao walifika kwa ajili ya kuhudhuria tukio hilo. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ATCL, kutokana na mabadiliko hayo ya hali ya hewa yamesababisha kubadilisha ratiba ya safari ya ndege hiyo ambayo ipo Marekani na ilitarajiwa kupokewa Zanzibar.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum, alisema taarifa ya kusita kufanyika kwa uzinduzi wa ndege hiyo imetokana na changamoto ya hali ya hewa na wananchi watelezwa lini ndege hiyo itapokewa.

"Kweli leo tulikuwa na mapokezi ya ndege mpya, lakini kutokana na hali ya hewa huko Marekani ndege imeshindwa kusafiri na kuja hapa, tunasubiri taarifa ya hali ya hewa itakapotengamaa tutawaarifu ndege itafika lini na wakati gani," alisema.

Ujio wa ndege hiyo mpya ya masafa marefu kunaiwezesha ATCL kuwa na jumla ya ndege 16, kati ya hizo 15 ni mpya ambazo zimenunuliwa kutokana na mpango wa ufufuaji wa shirika hilo ulioanza kutekelezwa mwaka 2016 na moja ni ya zamani, saba zimenunuliwa katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita.

# Mufindi yatenga mil. 458/- mikopo asilimia 10

**Na Agustino Kihombo, IRINGA**

HALMASHAURI ya Mji wa Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa, imetenga zaidi ya Sh. milioni 458 kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 itakayotolewa kwa wanawake, watu wenye ulemavu na vijana.

Mikopo hiyo inatarajiwa kutolewa kwa mujibu wa utaratibu mpya uliowekwa na serikali baada ya kusitishwa Aprili, 2023 na kutangaza kuanza upya mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Mipango na Uratibu wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Peter Ngusa katika baraza la madiwani la halmashauri hiyo, kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 halmashauri imetenga Sh. milioni 458 kwa ajili ya kuwainua wananchi kiuchumi.

"Sisi kama halmashauri tumejipanga kutekeleza takwa la kisheria linalotutaka tutenge asilimia 10 ya fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hadi sasa tunapozungumza tayari halmashauri imeshaingiza fedha hizo kwenye mfuko kwa ajili ya mikopo na tunasubiri maelekezo ili fedha ziweze kutoka," alisema Ngusa.

Katika hatua nyingine, Ngusa alisema namna halmashauri hiyo ilivyofanikiwa katika ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2023/2024, ambapo walikusanya kiasi cha Sh. bilioni 6.2 sawa na asilimia 113 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 5.5 jambo lililorahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Halmashauri yetu imeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo kwa mwaka uliopita tulikusanya kwa asilimia 113 zaidi ya lengo lililowekwa, hii inatokana na ushirikiano baina ya wataalamu na madiwani pamoja na viongozi wetu wa halmashauri katika kuhamasisha wananchi kulipa mapato na kuacha tabia ya kukwepa, jambo hili linaendelea kutupa mafanikio katika kukusanya mapato," alisema.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Elius Msuya akizungumzia awamu mpya ya mikopo hiyo inayotarajia kuanza kutolewa hivi karibuni, alisema moja ya changamoto iliyojitokeza katika awamu iliyopita ni urejeshaji hafifu wa mikopo hususani vijana kwa kuwa baadhi yao wanapopata mikopo hiyo hufanyia matumizi nje ya lengo mahususi

"Mikopo hii inatolewa bila riba kama utakopa milioni tano unarejesha milioni tano, lakini ni muhimu kujua kwamba unapochukua mkopo huu kuelekeza kwenye miradi yenye tija na sio kuchukua ili mgawane, ipo miradi mingi mnaweza kufanya na mkapata faida na mkafanikiwa kurejesha," alisema Msuya.

Aidha, alisema miradi inayotokana na mikopo hiyo ni muhimu kwa vijana na wanufaika wote kuwashirikisha wataalamu waliopo katika maeneo yao ili waweze kuzalisha kwa tija ikiwa ni pamoja na nidhamu ya fedha na umoja katika vikundi vyao.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Dk. Linda Salekwa, aliitaka halmashauri kujikita kutoa mikopo ya vifaa na vitendea kazi badala ya kutoa fedha, hii inafanya wengi wao kutumia fedha hizo kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

"Kama tulivyokubaliana kwenye Kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC), kwamba ifike mahali tuache kugawa mikopo kama ilivyozoeleka huko nyuma na badala yake tuwe na maeneo yetu ya vipaumbele kwa maana fedha hiyo iliyotengwa ni hakika kwamba inakwenda kubadilisha maisha ya wananchi, hivyo niombe tutoe mkopo na tuwape elimu ya bidhaa wanazoweza kuzizalisha ili zikiingia sokoni ziuzike," alisema Dk. Linda.

Aidha, alisema moja ya njia zitakazowawezesha wanufaika wa mkopo huo kukua kiuchumi ni pamoja na kujua nini wanatarajia kuzalisha na uhakika wa upatikanaji wa soko la bidhaa zao hayo yatasaidia kuwafanya wazalishe zaidi kwa tija, lakini pia kupata fedha za kurejesha madeni yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wakiwajibika ipasavyo kero za wananchi zitatatuliwa

**KILA** mara Rais Samia Suluhu Hassan anapofanya mabadiliko ya viongozi katika ngazi mbalimbali na kuwaapisha wateule hao, amekuwa akiwasisitiza kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Pia amekuwa akiwataka kuwa wabunifu katika kutatua kero zinazowakabili wananchi.

Sambamba na hayo, Rais Samia amekuwa akiwakumbusha wateule hao wakati wa kuwaapisha na kila anapofanya ziara mikoani kwamba wasijifanye miungu watu kwa kunyanyasa wananchi na kusujudiwa bali watambue kuwa ni watumishi wa wananchi. Kwa mantiki hiyo viongozi hao wamekuwa wakisisitizwa kutokukaa ofisini badala yake waende kwa wananchi kusikiliza kero zinazowakabili na kuzitatua.

Licha ya maagizo hayo, baadhi ya wateule hao wamekuwa wakidaiwa kutumia nafasi zao vibaya kwa kuwanyanyasa wananchi huku muda mwingi wakikaa ofisini badala ya kwenda kusikiliza kero na kuzitatua.

Hata hivyo, wako baadhi ya viongozi ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika utatuzi wa kero za wananchi kama vile ubovu wa miundombinu, uhaba wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo, migogoro ya ardhi na upatikanaji wa maji safi na salama. Wateule hao, akiwamo mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, wameonyesha mfano katika kushughulikia kero za wananchi na zingine kuzipatia ufumbuzi.

Kiongozi huo aliporipoti Arusha kuanza majukumu yake, alitembelea halmashauri zote na kubaini matatizo mengi yanayowakabili wananchi na kuhoji baadhi ya watendaji kwa nini wameshindwa kutafutia ufumbuzi. Kwa ujumla, mambo aliyoyaibua katika ziara yake hiyo, yalionesha kwamba watendaji wengi wameshindwa kutekeleza wajibu wao kwa kusimamia kazi zao pamoja na kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi.

Moja ya kero aliyoiibua na kuanza kuishughulikia ni migogoro ya ardhi huku baadhi ya wananchi wakilalamika kuwa baadhi ya watendaji kwenye sekta hiyo wamekuwa sehemu ya matatizo hayo.

Aidha, Makonda katika kampeni ya upimaji wa afya ambayo ilifanyika katika mikoa yote, alikuja na ubunifu wa kipekee kwa madaktari bingwa kutoka mkoani humo na taasisi kubwa kama Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Dk. Peter Kisenge, kwa ajili ya kufanya uchunguzi na kutoa tiba. Pia ziliandaliwa helikopta kwa ajili ya kuwapeleka wagonjwa waliobainika kuwa na maradhi makubwa yanayohitaji matibabu ya kibingwa kwenye hospitali kubwa.

Ubunifu huo ulipongezwa na viongozi wa ngazi ya juu akiwamo Rais Samia kuwa ni mfano wa kuigwa kwa viongozi wengine. Kwa hakika ubunifu kama huo ni chachu kwa viongozi mbalimbali, kwa nafasi zao, kufanya kile kinachotakiwa katika kutatua kero za wananchi.

Kumekuwa na msemo kwamba kama wao wanaweza kwa nini sisi tushindwe? Kutokana na msemo huo, ni kwa nini mtu mmoja aoneshe kwamba utatuzi wa kero unawezekana na wengine wanashindwa? Aidha, kwa nini wateule hao wamekuwa wakisisitizwa katika awamu zote za uongozi wa nchi kuwa wabunifu na kutambua kuwa ni watumishi wa wananchi na si watu wa kutumikiwa lakini wameshindwa kutekeleza maagizo hayo?

Ni wazi kwamba kutokupatikana kwa suluhu ya kero zinazowakabili wananchi, kunatokana na baadhi ya wateule hao kujiona kuwa miungu watu na wamezipata nafasi hizo ili kujinufaisha badala ya kumsaidia Rais kushughulikia matatizo ya wananchi.

Ni wakati mwafaka sasa wateule wa Rais, kwa maana ya wakuu wa mikoa na wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watendaji walio chini yao, wakarejea maagizo wanayopewa katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kwamba kero nyingi za wananchi zitapatiwa ufumbuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kuwa makini usipande maua kiholela ni hatari

**KUPANDA** maua ni njia mojawapo ya kupendezesha mazingira nyumbani, mitaani na mijini. Kutokana na hilo, karibu kila penye maeneo hayo watu wamepanda maua ya aina mbalimbali.

Pamoja na kwamba maua ni mapambo katika miji na nyumbani, tahadhari inatolewa kwamba ni vyema kuwa makini na maua ya kupanda nyumbani ili kuepusha madhara ya kiafya yanayotokana na mimea hiyo.

Msimamizi wa kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu (NPCC), kilichopo Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Yohana Goshashy, anaitahadharisha jamii kuhusu kupanda maua kiholela.

Yohana anasema kabla ya kuchukua hatua za kupendezesha mazingira ya nyumbani, ni vyema kuwaona wataalam wawaoneshe maua ambayo hayana madhara.

Kwa nini? Kwa sababu baadhi ya mimea hiyo inaweza kusababisha mzio kwa watoto, hasa wakigusisha na sehemu kama macho na mdomo, wanaweza kuwashwa macho na midomo kuvimba.

Pia wengine kulazwa hospitalini na hata kupoteza maisha endapo wakitafuna mbegu za maua hatari.

Hivyo jamii inatahadharishwa na kutakiwa kuwa makini kwenye suala la upandaji wa maua nyumbani.

Katika ufafanuzi wake, mtaalamu anasema maua mengi yana majina ya kisayansi na ya Kiswahili au Kiingereza ambayo wengine wanayatumia kwa tiba pia na urembo, akisema mnyonyo na kwamba unaweza kusababisha kifo.

> **Hivyo, kwa elimu ya mtaalam huyo, itoshe kutufundisha kitu, ili kama ikiwezekana, tutumie nafasi kubwa kupanda miti ya kivuli na matunda pembeni mwa nyumba zetu badala ya kurundika maua**

Ni wakati wa wale wanaopenda kupanda maua nyumbani au maeneo wanakocheza watoto kuchukua hatua zinazoshauriwa.

Ni kweli mimea ya maua mbalimbali ni mapambo yanayopendezesha makazi lakini suala la kuchukua tahadhari, kulinda afya ni la muhimu, ili kupanda mimea isiyo na madhara kiafya.

Katika jamii, watu wanajenga nyumba zao na kuzipamba kwa maua mengi yanayonukia, na kumbe ndani ya hiyo harufu nzuri kuna hatari ambayo inaweza kumkuta mpandaji bila kujua.

Hivyo, kwa elimu ya mtaalam huyo, itoshe kutufundisha kitu, ili kama ikiwezekana, tutumie nafasi kubwa kupanda miti ya kivuli na matunda pembeni mwa nyumba zetu badala ya kurundika maua.

Ninaamini kwamba asilimia kubwa ya watu, watakuwa hawana elimu kuhusu madhara yanayotokana na maua, kwani lengo la kupanda ni kutaka kupendezesha mji si kuleta kuumiza familia.

Kwa maana hiyo, kama itawezekana, ninadhani ni vyema jamii ikaelimishwa kwa upana zaidi kuhusu utunzaji wa mazingira ya nyumbani, hasa kwa upande wa upandaji wa maua.

Ni kawaida kwenda katika mji na kukuta umepambwa na maua ya aina mbalimbali, lakini inapokuja taarifa kuwa yapo baadhi ya maua ni hatari kiafya. Hii ni taarifa mpya ambayo ni vyema jamii ikaipata kwa undani.

Iwapo jamii itakuwa na uelewa wa kutosha, itakuwa ni rahisi kutambua maua hatari na yale ambayo hayana madhara, na itakuwa ni rahisi kuyatambua na kuyaepuka haraka.

Vinginevyo, watu wanaweza kuendelea kuumia bila kujua chanzo chake. Lakini wakionyesha maua hatarishi itakuwa ni rahisi kuchukua hatua ya kuachana nayo badala ya ilivyo sasa.

Kinachotakiwa, ni kujua aina ya maua ambayo unayo nyumbani kwako kama kuna yenye sumu uyaondoe haraka iwezekanavyo kabla hayajasababisha madhara kwako au familia yako.

Hiyo inategemea elimu ambayo atakuwa amepewa na wataalam wa mambo ya maua, na kama itashindikana, basi ni vyema watu waelekeze nguvu pia kwenye kupanda mboga.

HABARI KITAIFA

# Msichana Initiative yamwandikia barua Rais Samia kutaka maboresho Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Msichana Initiative limesema limemwandikia barua Rais Samia Suluhu Hassan, likimwelezea kuhusu kusuasua kwa mchakato wa kufanyiwa maboresho vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Kwa mujibu wa Ofisa Uchechemuzi wa Shirika hilo, Jacob Maduki, wameamua kumwandikia barua Rais Samia ili afahamu kinachoendelea katika suala hilo ambalo licha ya mahakama kuamuru sheria hiyo ifanyiwe mabadiliko tangu mwaka 2019, lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika.

"Baada ya mahakama kutoa hukumu mwaka 2019, ilitakiwa baada ya mwaka mmoja ifanyiwe mabadiliko, lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika na hakuna sababu za msingi zinazotolewa," alisema Maduki.

"Na tumekuwa tukifuatilia kwenye mamlaka husika ikiwamo bunge, lakini hakuna majibu ya msingi yanayotolewa na ndio maana tukaamua kuandika barua kwenda kwa Rais ili afahamu hili maana tunaamini ni mpenda haki ataliona hili."

Kifungu cha 13 cha sheria hiyo ya ndoa, kinaeleza kuwa, wavulana na wasichana wanaweza kuoa au kuolewa wakiwa na umri wa miaka 14 kwa idhini ya mahakama.

Wakati kifungu cha 17, kinaeleza kuwa ndoa ya msichana mwenye umri wa miaka chini ya 18, anaolewa kwa idhini ya wazazi wake na kama hakuna wazazi, idhini itatolewa na walezi na kama wote hao hawapo hakuna idhini yoyote, ataolewa.

Makudi alisema mbali na kuandika barua hiyo kwenda kwa Rais, pia wanaendelea kutoa elimu katika makundi mbalimbali ya jamii ikiwamo kwa viongozi wa dini ili kuwaelewesha kwa kina athari zinatowapata watoto kutokana na kuozwa au kuolewa wakiwa na umri mdogo.

Wakili kutoka Shirika hilo, Lucy Didamisi, alisema wamefuatilia mara kadhaa kwenye mamlaka zinazohusika na kubadilisha sheria ikiwamo kurudi tena kuulizia mahakamani na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini majibu walipatiwa kwamba wao wamefanya kwa sehemu yao na kazi iliyobaki inatakiwa kufanywa na mamlaka husika.

Shirika la Msichana Initiative kupitia kwa Mkurugenzi wake, Rebecca Gyumi, lilifungua shauri Mahakama Kuu ya Tanzania kwa niaba ya watoto wote walio katika hatari ya kuingia kwenye ndoa za utotoni la madai namba (5) ya mwaka 2016 kupinga uhalali wa kikatiba wa ndoa za utotoni.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) Halima Mdee akiongoza kikao cha kamati hiyo kwenye vikao vya kamati vinavyoendelea Bungeni Dodoma jana .. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

# Hospitali zasisitizwa gharama stahimilivu

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa sekta binafsi wanaojihusisha na utoaji wa bima ya afya nchini wametoa wito kwa hospitali mbalimbali nchini kuacha kuweka gharama kubwa za matibabu badala yake waweke viwango ambavyo vitakuwa stahimilivu kwa Watanzania wa hali zote.

Wito huo ulitolewa jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya (ishi huru) itakayoendeshwa katika nchi tatu ikiwamo Tanzania, Kenya na Uganda ikilenga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima ili kuwasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Afya ya Jubilee, Dk. Harold Adamson, alisema uelewa wa matumizi ya bima nchini ni chini ya asilimia moja, wadau mbalimbali wanapaswa kujua kuwa wana kazi kubwa ya kufanya ili kuchochea Watanzania wa hali zote kujiunga na bima ya afya.

"Pia, ni maombi yetu kwamba wale wanaotoa huduma kule hospitalini wanapowahudumia wawekee gharama ambazo ni stahiki, iwe ni 'reasonable amount' anapoenda huduma ya kumuona daktari iwe ambayo ni stahimilivu kwa maana ya kila Mtanzania awe na uwezo wa kulipa," alisema na kuongeza:

"Wale Watanzania wangeweza kulipa kule 'cash' lakini wameona wapitie kwenye bima basi hospitali ziweze kutambua kwamba hizi ni fedha za watu zimewekwa kwenye 'pull' moja ili ziweze kumhudumia yule ambaye anaumwa kwa wakati ule na sio 'kuzitapanya'," alisisitiza Dk. Adamson.

Pia, alisema kuwa lengo la fedha hizo ni kutoa huduma kwa watu na wamekuwa wakiheshimu uhusiano wao na wadau wa afya, pamoja na kuzingatia ulipaji wa fedha kwa wakati na vizuri katika hospitali baada ya mwananchi kupatiwa huduma.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi na taasisi za bima ya afya kufanya kazi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan siku chache zilizopita kusaini muswada wa bima ya afya kwa wote, ambao iliwapa nafasi ya kuwa wabunifu na kutengeneza bidhaa mbalimbali ili kumfikia mwananchi wa chini.

Naye, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life, Helena Mzena, alisema umuhimu wa kampeni hiyo ni kutoa elimu na kuendeleza uelewa kwa wananchi kujua matumizi sahihi ya bima.

"Kuna dhana iko kwamba bima ni ya watu fulani, lakini hii ni kwa ajili ya kila mtu kwa sababu wote tunaugua hakuna mkubwa wala mdogo, hivyo ni muhimu kujua na kuwa na uelewa kuwa bima inaweza kumkinga vipi pale inapotokea ameumwa, ili waweze kufanya shughuli zao kwa uhuru," alisema Helena.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Kunenge aahidi kuwashughulikia makandarasi wazembe

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amesema hayuko tayari kuvunja mikataba na makandarasi badala yake malalamiko yakizidi kutokana na mradi unaotekelezwa atamshughulikia moja kwa moja anayehusika.

Kunenge aliyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akishuhudia utiaji wa saini mikataba ya ujenzi wa barabara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

"Sina uwezo wa kuvunja mikataba ila kama hutekelezi vizuri wananchi wanalalamika na hali ya usalama ikawa mbaya nitakushughulikia katika eneo hilo ila sio kuvunja mkataba wako," alisema.

Kadhalika, alisema endapo mkandarasi katika ujenzi wa barabara atakuwa na kikwazo ni vema akakutana naye moja kwa moja kabla ya mambo hayajaharibika ili utatuzi ufanyike mapema.

Pia, alisema makandarasi hao wanatakiwa kufanya kazi kwa mujibu wa mikataba yao na kuwashirikisha wakuu wa wilaya kwenye maeneo yao.

"Rais akipita kwenye mkoa wetu apokewe kwa kushukuriwa kutokana na miradi iliyotekelezwa kwa ufanisi na sio malalamiko ya wananchi kwa miradi iliyopatiwa fedha," alisisitiza Kunenge.

Mkuu wa Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Hadija Nasri alisema ni vema wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo wakazingatia taratibu na kulipa kodi inayotakiwa ambayo itakwenda kutatua baadhi ya kero za wananchi.

Awali, akitoa taarifa ya mikataba hiyo, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Pwani, Mhandisi Leopold Runji alisema katika mwaka wa fedha 2024-2025 wameidhinishiwa Sh. bilioni 31.475.

Mhandisi Runji alisema fedha za mfuko wa barabara zinatengemea kufanya matengenezo ya kawaida kwa kilomita 810, matengenezo ya sehemu korogi 338.56, matengenezo ya vipindi maalumu kilomita 77.34, ujenzi wa makaravati mistari 80 na boxing karavati tatu.

Alisema fedha zitokanazo na tozo ya mafuta zitakwenda kujenga barabara kiwango cha lami kilomita 1.75, ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe kilomita 203.87, boksi kalavati saba na makaravati mistari 27.

Mhandisi Runji alisema fedha nyingine ni kutoka Mfuko wa Jimbo na za miradi ya maendeleo ambazo zitajenga barabara kiwango cha changarawe na kiwango cha lami.

# Bil. 4/- kupeleka umeme mgodi wa makaa ya mawe

**Na Gideon Mwakanosya, MBINGA**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 4.6 kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya migodi mkoani Ruvuma na Sh. milioni 280 zimepelekwa katika mgodi wa Market Insight Limited (MILCOAL), uliopo katika Kijiji cha Paradiso, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani humo.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa kituo cha mauzo cha makaa ya mawe ya Kampuni ya Market Insight Limited Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alisema tayari wameshaanza kupeleka umeme, nguzo zimeshawekwa na wameshaanza kuvuta waya na kuahidi ndani ya mwezi mmoja utafika eneo la mgodi.

Aidha, alisema kuwa anawapongeza Market Insight Limited kwa jitihada za kuendelea kuimarisha utulivu ndani ya mgodi kiuchumi na uwezeshwaji wa kiuchumi kupitia fursa zinazopatikana, ikiwamo fursa za ajira na uwekezaji huo unaendelea kuchochea uchumi wa taifa.

"Nawapongeza sana MILCOAL kwa kuendelea kuwekeza pamoja na fursa mbalimbali kwaajili ya kuendeleza uwekezaji huu katika mgodi, ninyi ni mfano wa kampuni zinazofanya vizuri kwenye kuendeleza fursa za uwekezaji, nafahamu vituo vya usambazaji wa madini ya makaa ya mawe vipo mbali na migodi.

"Pamoja na sababu zingine mojawapo ni changamoto ya barabara, natambua kuwa kama uwekezaji wa mwanzoni mliweka mazingira mazuri, ikiwamo kufungua barabara kutoka sehemu ya Kijiji cha Mtunduwalo hadi Luwimbi kwa gharama ya Sh. milioni 800," alisema Naibu Waziri wa Nishati Kapinga.

Aidha, alisema kuwa, japo barabara hiyo bado ina changamoto, lakini wanatambua jitihada hizo za mwanzoni ambazo zimewanufaisha watu wengi, ikiwamo wawekezaji wengine wa migodi na serikali inaendelea kukwamua ujenzi wa barabara hiyo.

Alisema pia barabara zote zinazoingia katika maeneo ya migodi, Waziri wa Ujenzi alishafika katika eneo hilo na amewahakikishia linaendelea kufanyiwa kazi na wakati wowote kuanzia sasa shughuli za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami utaanza.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alisema sekta hiyo ndogo ya makaa ya mawe ina mchango mkubwa katika usalama wa nishati uwekezaji wa viwanda vya ndani na nje ya nchi.

Alisema halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ni mojawapo ya maeneo muhimu yanayochangia uwekezaji kupitia madini hayo kwa kiasi kikubwa.

Awali akisoma taarifa ya mradi huo, mwakilishi wa Kampuni ya Market Insighht Limited, Mussa Hadji alisema kampuni hiyo ilianza rasmi shughuli za uchimbaji wa madini ya makaa ya mawe 2017 katika Wilaya ya Mbinga, mkoani Ruvuma kwa lengo la kuchangia kikamilifu sekta ya madini nchini.

Aidha, kupitia uchimbaji na uuzaji wa makaa ya mawe tangu kuanzishwa kampuni hiyo imejipambanua kwa kuzalisha na kusambaza makaa ya mawe yenye ubora wa hali ya juu kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Peles Magiri, alisema kuwa kupitia usimamizi thabiti wa serikali miundombinu muhimu kama ya barabara na usambazaji wa umeme katika maeneo ya migodi vimeendelea kuboreshwa hali itakayorahisisha uendeshaji wa shughuli za kibiashara na kuboresha upatikanaji wa nishati kwa urahisi kwa watumiaji pamoja na juhudi kubwa zinazotekelezwa na serikali.




Diwani wa Kata ya Kivukoni, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Sharik Choughule akiwa katika kilele cha Mlima Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mavunde aziomba benki kuiunga mkono CRDB kukopesha wachimbaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wakiwamo wadogo na kuzitaka benki na taasisi nyingine za fedha kuiga mfano huo.

Waziri Mavunde alitoa kauli hiyo jana mjini Kahama alipokabidhiwa ripoti ya utoaji huduma za fedha kwa wachimbaji wadogo na wa kati kutokana na maelekezo aliyoyatoa mwaka jana alipokutana na watendaji wa benki za biashara nchini.

"Wachimbaji wadogo ni jeshi kubwa kwenye sekta ya madini nchini, lakini lenye changamoto ya mtaji. Iwapo benki zetu za ndani zitawapa kipaumbele watu hawa kama mnavyofanya Benki ya CRDB, mchango wa sekta ya madini kwenye pato letu la taifa utaongezeka kwa kiasi kikubwa. Nawapongeza Benki ya CRDB kwa kuona umuhimu wa kuizingatia sekta hii," alisema Waziri Mavunde.


Mwaka jana, Mavunde aliwaeleza watendaji wa benki nchini kuhusu changamoto ya upatikanaji wa huduma za fedha ikiwamo mikopo kwa wachimbaji wadogo na kuwataka kuangalia namna ya kurahisisha upatikanaji wake ili kukuza mchango wa sekta ya madini nchini ambayo inaajiri maelfu ya wananchi katika mikoa mbalimbali nchini.

Mavunde alisema serikali itandelea kuimarisha mazingira ya uchimbaji nchini ikiwamo kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo kufanya utafiti utakaowasaidia kuchimba maeneo yenye uhakika wa kupata madini tofauti na hali ilivyo sasa wanapochimba kwa kubahatisha.

"Serikali inaendelea na juhudi za kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kutekeleza mikakati tofauti kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) pamoja na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa kuwa inatambua kuwa bado wachimbaji wadogo wengi wanafanya shughuli zao bila kufanya utafiti wa kisayansi hivyo kutokuwa na uhakika wa kupata madini wanayoyakusudia," alisema.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alimjulisha kuhusu hatua kadhaa zilizofanywa na benki hiyo katika kuwawezesha wachimbaji wadogo pamoja na changamoto ilizokutana nazo.

Akiainisha mchango wa Benki ya CRDB, Raballa alisema imeanzisha kitengo maalum cha madini ili kutoa wigo mpana wa utekelezaji wa mikakati inayoelekezwa kwenye sekta ya madini na kujenga uwezo kwa wafanyakazi kuchambua maombi na mahitaji ya wachimbaji wadogo wa madini.



# H'shauri ya Babati yavuka lengo uandikishaji wanafunzi awali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani hapa imevuka lengo kwa kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali 3,695 kwa zaidi ya asilimia 100.

Akizungumza na Nipashe juzi Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Simon Mumbee, alisema kati ya wanafunzi hao, wavulana ni 1,900 na wasichana ni 1,795.

Mumbee, alisema makisio yao ilikuwa kuandikisha wanafunzi 3,641 wakiwemo wavulana 1,879 na wasichana 1,762 hadi kufikia Machi 31 mwaka huu.

Alisema walivuka lengo hilo kwa kushirikiana na viongozi wa mitaa, kata, walimu na wazazi.

Ofisa elimu huyo, alisema idadi ya wanafunzi wa awali wanaoandikishwa kuendelea na masomo hadi darasa la saba imeongezeka kutokana na wengine kuhamia.

Alisema kupitia programu ya Boost, inayolenga kuboresha elimu ya msingi, imesaidia maeneo manane ikiwemo uandikishaji wa darasa la awali na darasa la kwanza.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2014, serikali itaweka utaratibu wa elimu ya awali kuwa ya lazima na kutolewa kwa watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi mitano kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.

Na kwa mujibu wa mtaala na muhtasari wa elimu ya awali mwaka 2023, uwiano wa mwalimu kwa watoto unapaswa kuwa mmoja kwa wanafunzi 25.

Mkazi wa Mtaa wa Kwere, Halima Abdul, alisema suala la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali halina ubishi kwa kuwa mwanafunzi ndio anakuwa anaanza shule na wengi wanakuwa na shauku ya kusomesha.

Mkazi wa Mtaa wa Nyunguu, John Paschal, alisema wazazi wengi hawana ubishi kuandikisha watoto wa darasa la awali kwa kuwa walimu wanawasaidia kulea watoto hao.

Mshauri wa Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) wa Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka, akizungumzia mafanikio ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali, alisema kuongezeka kwa uandishikishaji wanafunzi hao kwa halmashauri hiyo kutoka asilimia 75 Januari 23 mwaka huu mpaka asilimia 101 Machi 31 mwaka huu kunaonyesha uelewa wa wazazi ni mkubwa.

Gisuka, alisema baada ya mafanikio hayo,ni vizuri kujua mwisho wa mwaka kama wanafunzi wote watavuka kwenda darasa la kwanza wakiwa na umahiri.

## STAMICO wawaunga mkono Wanawake na Mama Samia

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKURUGENZI wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk.Venance Mwase amesema wameanzisha nishati mbadala ya rafiki kwa ajili ya matunzi ya nyumbani ili kuhakikisha wananchi wanalinda, kuhifadhi na kutunza mazingira nchini.

Dk. Mwase aliyasema hayo juzi wakati akishiriki kampeni ya upandaji wa miti katika eneo la Amboni jijini Tanga iliyoratibiwa na Wanawake na Samia Mkoa wa Tanga kwa lengo la kutambulisha nishati hiyo safi mbadala inayojulikana kwa jina la Briquettes.

Alisema katika kufanikisha hilo, watazuia ukataji miti na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo.

"Suala la nishati safi ya kupikia ni ajenda ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, niwapongeza Wanawake na Samia Mkoa wa Tanga kwa kuunga mkono ajenda hiyo na sisi tutaendelea kuwaunga mkono," alisema Dk. Mwase

Alisema wana wajibu wa kutunza mazingira kwa kutafuta njia mbadala yasiharibiwe na wananchi kwa kuwa wengi wao bado hawana nishati mbadala na wanatumia kuni na mkaa ambao unatokana na miti.

Alisema kupitia programu hiyo, wamelenga kuhamasisha upandaji miti ili kuzuia uharibifu na ndio sababu wametafuta nishati mbadala ya kupikia.

Dk. Mwase, alisema ili kuhakikisha nishati mbadala inapatikana kukidhi mahitaji ya wananchi na kutunza mazingira, wamefikia hatua ya kuitambulisha nishati hiyo.

"Utafiti umekamilika na uzalishaji umeanza na Wanawake na Samia watakuwa wauzaji pamoja na kuhamasisha matumizi hayo kwa kinamama kwa kuwa wao ndio wanaathirika na watafutaji wa nishati," alisema.

Dk. Mwase alionya kuwa mazingira yakiharibiwa na kuathiriwa, wananchi watashindwa kulima mazao, kupata hewa safi na kuwa janga kwao na taifa.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bonde la Mto Pangani, Michael Buli, alisema watakuwa bega kwa bega na wananwake hao kutunza mazingira na vyanzo vya maji ili kufanikisha kampeni hiyo.



Watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani wakifurahia mlo wa mchana katika eneo la Shira ndani ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro wakati wa safari yao ya kuelekea katika kilele cha juu kabisa cha mlima huo maarufu kama 'Paa la Afrika' mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: JAMES LANKA**

## Walimu, wanafunzi wajisaidia vichakani

**Na Steven William,** MUHEZA

WANAFUNZI wapatao 437 na walimu 11 wa shule ya msingi Kwelubuye na Paramba zilizopo Kata ya Kicheba wilayani hapa Mkoa wa Tanga wanalazimika kujisaidia vichakani na nyumba za wenyeji kwa kukosa vyoo.

Hayo yalisemwa wiki iliyopita na Diwani wa Kicheba, Hamis Mkodingo wakati akiwasilisha kero ya shule hizo katika kikao cha baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Akiwasilisha kero hiyo, Mkodingo alimuomba Mkurugenzi wa halmashauri hiyo kujenga matundu ya vyoo katika shule hizo ili kuondoa aibu kwa walimu na wanafunzi wake kujisaidia vichakani na nyumba za wenyeji.

Akijibu kero hiyo na nyingine zilizowasilishwa na madiwani katika kikao hicho, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Salimu Sechambo alisema wamezisikia na kuahidi kuzishughulikia.

## Wananchi wakerwa ujenzi barabara kusuasua

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Mabogini wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wameiomba Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mabogini-Kahe na kuwaondolea kero wanazopata mvua zinaponyesha.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi hao, Yusufu Kassim, alisema kuchelewa kukamilka kwa ujenzi wa barabara hiyo ni kero kwao, ikiwemo maji kutuama, kugeuka dimbwi na kushindwa kupitika.

Kassim, alisema licha ya serikali kutoa ahadi nyingi tangu mwaka 2015 ukarabati wa barabara hiyo bado umeendelea kusuasua na kuwa kero kwao.

"Barabara hii ni tatizo kwa vyombo vya moto kwani vinaharibika mara kwa mara, barabara hii inatuongezea umasikini na kukatisha uhai wa maisha ya baadhi yetu.

"Wapo wajawazito wanapokwenda hospitali hasa nyakati za mvua na wagonjwa hupoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma ya kuwahishwa hospitalini mapema kutokana na ubovu wa barabara hii, " alisema mkazi mwingine, Zulpha Musa.

Zulpha, alisema hawaoni faida ya wakandarasi na viongozi wa serikali kutembelea na kukagua barabara hiyo kutokana na kushindwa kukamilisha ukarabati.

"Tunaona mkandarasi kashindwa kazi kwa kuwa tuliambiwa fedha za kujenga barabara zimetolewa na Benki ya Dunia (WB), " alisema Rukia Ahmed.


Kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 32, ulianza Juni mwaka huu na kutarajiwa kukamilika Februari mwakani

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Africano Orotha, alisema wamepokea Sh. milioni 475 kwa ajili ya kukarabati eneo korofi na kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami.Kwa mujibu wa Orotha, katika mwaka huu wa fedha wa 2024/25, watakarabati barabara hiyo kipande cha mita 800 kwa kunyanyua tuta na kujenga mitaro ya maji ya mvua.

"Katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha, TARURA imetenga Sh.milioni 475 kwa ajili ya kutengeneza kipande cha lami kingine cha mita 800," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu,alisema wanatambua adha wanazopata wakazi hao na kuwaomba kuwa wavumilivu wakati serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha ujenzi huo.

"Tumepokea maelekezo maalumu ya ujenzi wa barabara korofi kutoka kwa Waziri Mkuu, Kassim Kassim Majaliwa kuhusiana na matengenezo ya barabara korofi, tunaomba wananchi kuwa wavumilivu wakati tunaendelea kufanyia kazi suala hili," alisema Babu.





## 'Acheni kulima bangi'

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKUU wa Wilaya ya Tarime Mkoa wa Mara, Maulid Surumbu amewataka wakulima wilayani hapa kujiinua kiuchumi kwa kuchangamkia kilimo cha tumbaku na kuachana na cha zao haramu la bangi.

Surumbu alitoa rai hiyo katika Mkutano wa Chama cha Wakulima Mkoa wa Mara (WAMACU) wa kuwajengea uwezo wakulima, maofisa ugani na viongozi wa serikali kuhusu mbinu bora za kilimo cha zao hilo.

Alifafanua kuwa ametoa rai hiyo baada ya bei ya tumbaku kuongezeka kutoka Shilingi 4,625 hadi 6,100

Meneja Mkuu wa WAMACU, Samwel Gisiboye, alisema kwa msimu wa mwaka uliopta wa 2023/24, chama hicho kilisimamia zabuni za pembejeo ili kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mara, Lucas Kiondere, alisema WAMACU imejipanga kutatua kero zinazokabili kilimo hicho na kuandaa mafunzo yatakayoimarisha sekta hiyo.

Ofisa Kilimo wa WAMACU, Nightess Adonias, WAMACU alisisitiza umuhimu wa kutumia mbinu endelevu katika kilimo hicho ili kukabiliana na hali ya maisha na matumizi ya nishati mbadala kama vile umeme na nguvu za jua.

Kilimo cha tumbaku nchini kilianzishwa mwaka 1930, na kwa sasa zao hilo linalimwa katika mikoa 13, ukiwemo Mara na kuchangia kwa asilimia kubwa pato la Taifa na mtu mmoja mmoja.

**Meneja Mkuu wa WAMACU, Samwel Gisiboye, alisema kwa msimu wa mwaka uliopta wa 2023/24, chama hicho kilisimamia zabuni za pembejeo ili kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima.**

# Kanisa, viongozi CCM wataka amani kwenye uchaguzi nchini

**Na Samson Chacha,** TARIME

KANISA la Waadventista wa Sabato (SDA) nchini limetaka imani idumishwe katika uchaguzi wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu ili wananchi wachague viongozi bora watakaoleta maendeleo kwa taifa.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na kiongozi wa DSA nchini lenye makao makuu jijini Arusha, Mchungaji Mark Walwa Malekana katika maadhimisho ya Jubilee miaka 115 ya kuanzishwa kwa kanisa hilo iliyofanyika wilayani hapa Mkoa wa Mara.

Mchungaji Malekana, alisema kanisa hilo la Kibumaye ni moja ya makanisa kongwe katika mikoa ya Kanda ya Ziwa tangu kufunguliwa kwake mwaka 1909, likianzisha miradi ya maendeleo ikiwemo ya shule za msingi, sekondari na vituo vya afya.

"Bila amani hakuna maendeleo, hivyo tunahitaji kuilinda kwa nguvu zote hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika 2025,"alisema.

Mchungaji wa SDA Kibumaye, Isack Gama, alisema wameitwa wadau mbalimbali kufanikisha kuimarisha ujenzi wa kanisa hilo.

Aliwataja baadhi kuwa ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Daniel Chochori kwa kuchangia vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 3.6 ikiwemo mifuko ya saruji, mabati na nondo.

Josephat Isack Sh. milioni moja na wachangiaji wengine na kufanikisha kufikisha zaidi ya Sh.milioni 10.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Chonchori, aliwataka wadau kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

"Viongozi tuzidi kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari la wapiga kura na siku ya kupiga kura waende kupiga kura na kuwachagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo wananchi na sio wa maneno matupu kwenye majukwaa ya siasa, " alisema.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mara, Samwel Kiboye 'Nambatatu', alisema wananchi wanatakiwa kutanguliza amani, upendo, kuepuka ubaguzi wa dini, siasa na kabila.



Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima, akizungumza na wananchi juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika soko kuu la Singida. Katika mkutano huo aliwataka wafanyabiashara wanaopanga bidhaa zao katikati ya barabara kuzingatia maelekezo ya serikali ya kufanya biashara zao inapofika jioni. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mabinti waliokatisha masomo wajiajiri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya mabinti wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga waliokatisha masomo katika shule za msingi na sekondori kutokana na sababu mbalimbali, wamejiajiri na kuanza kujiinua kiuchumi, imefahamika.

Mabinti hao wamejiajiri baada ya kuhitimu katika fani za muziki, ushonaji, ususi, ufundi bomba, umeme, mitambo, uuguzi na ukunga katika chuo cha Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) Mwakata.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki iliyopita wakati mabinti hao wakionesha ujzi wao mbele ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka huu, Geofrey Mnzava.

Walisema walipatiwa mafunzo hayo katika chuo hicho chini ya ufadhili wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na UNFPA kupitia Mradi wa "Chaguo langu Haki yangu".

Mmoja wa mabinti hao, Naomi Emmanuel, alisema kwa sasa wamejikwamua kiuchumi tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya kupatiwa mafunzo hayo.

Naomi, alisema fani ya umeme aliyojifunza kupitia mradi huo, imemsaidia kujiajiri na kujiingizia kipato cha kumsaidia kuendesha maisha yake na wategemezi katika familia yake tofauti na awali.

Alilishukuru WiLDAF kwa kuwapatia vifaa kazi bure na kuwasaidia kujiajiri katika fani walizosomea VETA.

Elizabeth Alex, alisema mabinti wengi wanaotoka katika mazingira magumu wanashindwa kujiwezesha kiuchumi na kupitia wao watahakikisha wanawafikia na kuwaelimisha walichojifunza hasa ufundi cherehani ili waelimike na kujiajiri kama wao.

Kwa upande wake, Mnzava, alionesha kufurahishwa na hatua ya mabinti hao kujiajiri, akisemampango huo ni sehemu ya takwa la serikali kwa vijana kujishughulisha kwa kuanzisha miradi, kuajiri, kuajiri wengine na kuondokana na umaskini wa kipato kwa kukuza uchumi.

Alisema serikali imekuwa ikiwawezesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini kuwainua kiuchumi kwa kukuza mitaji yao na kuondokana na dhana ya kuitegemea kuwaajiri.

# Serikali yapeleka maji vijijini Ushetu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAKAZI wa vijiji vya Chona, Bukomela na Ubagwe vilivyopo Halmashauri ya Ushetu wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wameishukuru Serikali kwa kuwaondolea adha ya kukesha usiku kucha kusaka maji kwa ajili ya matumizi yao ya kila siku.

Shukrani hizo walizitoa mwishoni mwa wiki iliyopita wakati Mwenge wa Uhuru ukiweka jiwe la msingi ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji katika Kijiji cha Chona kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji safi na salama kwenye maeneo yao.

Mmoja wa wanavijiji hao, Neema Selemani, alisema mradi huo ukikamilika utawaondolea adha ya kuamka usiku na kwenda kutafuta maji safi na salama umbali mrefu na mradi huo.

Meneja wa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kahama, Mhandisi Maduhu Magili, alisema wamepokea Sh. bilioni 1.4 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo lengo likiwa ni kufikia lengo la kumtua mama ndoo kichwani.

Kwa mujibu wa Magili, mradi huo ambao ulianza kutekelezwa Februari 14, mwaka huu unatarajiwa kukamilika Novemba 11 mwaka huu na kunufaisha wananchi 5,763.

Alisema hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 55 na kwamba wamepewa jukumu hilo na serikali kusimamia hadi kukamilika kwake.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge huo kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Mnzava, alimtaka Meneja wa RUWASA kuhakikisha unakamilika kulingana na mkataba na wanakijiji hao kulinda miundombinu yake ili izidi kuwasaidia.

Nipashe
# TESA
Jumanne AGOSTI 20, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 13

## Mageuzi ya kielektroniki yawaunganisha wananchi,watoa huduma, vituo vya afya


Ukurasa 14

Wahitimu waandae cha kufanya baada ya kupata 'digirii' vyuoni,


Ukurasa 12

Kumbe oksijeni duniani chanzo ni bahari si anga, mimea kama ilivyodhaniwa awali

NA SABATO KASIKA

# Umbali mrefu kufika shule hauwaachi watoto salama

## Huenda ni kichocheo kutekwa, kunyanyaswa

MATUKIO ya watoto kupotea au wakati mwingine kubakwa na kuuawa yanaripotiwa sana, na hivi karibuni Mbagala jijini Dar es Salaam, ikiongoza kwa taarifa za kuhuzunisha.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, mwishoni mwa wiki alieleza kuwapo na matukio manne ya kuuawa watoto kadhaa eneo hilo.

Kwa mujibu wa Kamanda Murilo, kwa Mbagala pekee watoto wanne wameuawa kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja.

Watoto hao wadogo ambao baadhi yao ni wanafunzi wa shule za msingi, wanakumbana na matatizo mengi hasa wale ambao wanatembea wenyewe umbali mrefu bila uangalizi na wanaozurura mitaani.

Kwa mfano wanaosafiri kwenda shuleni. Wapo watoto wanaosoma kwenye shule zilizo mbali pengine hata kilometa 20, hawa ni 'wasafiri' kwa sababu muda mwingi wako barabarani, wana mabegi mazito mgongoni na pia wapo ambao hawana nauli wala chakula.

Inatokea wakasafiri kwa mabasi ya mijini au daladala ambazo mara nyingi zinawakataa. Tatizo hilo linachangiwa na wazazi na walezi kuwapeleka kwenye shule za mbali kwa lengo la kuwatafutia elimu bora katika shule wanazodai wanaziamini zaidi, hata kama ni za mbali.

Mfano, maeneo ya majijini, mijini na hata kwenye miji mikuu ya wilaya, baadhi ya wazazi na walezi hupeleka watoto wao kusoma shule za mbali na nyumbani kwa kutumia usafiri usioaminika kama malori ya mizigo, lifti za wasiowafahamu na daladala.


Watoto wakiwa na mabegi ya shule **PICHA:MTANDAO**

Wakati mwingine watoto wanakosa usafiri huo, kutokana na sababu kama magari hayo kutokuwepo hasa ya lifti, yale ya mizigo kuwakataa kama ambavyo makondakta wa daladala nao huwakwepa kwa sababu nauli ya ndogo.

Wakati mwingine watoto wa miaka sita hadi 10 husota vituoni kuanzia alfajiri na mabegi makubwa ya shule migongoni bila usafiri.

Lakini serikali imejenga shule za msingi nyingi za msingi, katika mikoa mbalimbali na ziko maeneo ya mijini na vijijini ili wanafunzi wasome karibu na nyumbani.

Kwa sasa unaweza kuona kuna shule ya msingi A na B, katika eneo moja. Cha kusikitisha ni wengi wa watoto wadogo kuanzia miaka sita wanaobebeshwa mabegi mgongoni yaliyojazwa madaftari na vitabu wanahangaika kutafuta usafiri kwenye daladala na hata kuangukia kwenye mikono ya wauaji na wanyanyasaji.

Kwa kuangalia matatizo na changamoto wanazopitia wazazi na walezi wawapeleke katika shule za jirani ili kuwapunguzia adha na unyanyasaji.

Mwalimu mstaafu, Suzan Lyimo, anazungumzia suala hilo, akisema, inawezakana kuna jambo ambalo wazazi na walezi wanalitafuta, linalosababisha watoto waenda mbali kufuata elimu.

"Haiwezekani wahangaike kumpeleka mtoto mbali huku kukiwa na shule jirani. Hapa kuna jambo haliko sawa," anasema Suzan, anapozungumza na Nipashe.

Anafafanua kuwa wakati mwingine shule inawezakana kuwa haina walimu au wapo lakini hawafundishi inavyotakiwa.

"Katika mazingira hayo, hata mimi siwezi kupeleka wanangu kwa sababu hawawezi kusoma kikamilifu," anasema mwanasiasa na mbunge mstaafu wa CHADEMA .

Anaongeza kuwa walimu kutofundisha ipasavyo au kuwa wachache ni usumbufu kwa wanafunzi, wazazi na walezi na

INAENDELEA UK.12

# Umbali mrefu kufika shule hauwaachi watoto salama

INATOKA UK.11

wakati mwingine wanalazimika kutafuta 'twisheni'.

Mdau huyo wa elimu anaitaka serikali kufuatilia na kuondoa kero hiyo inayowakumba wanafunzi lakini pia ikiongeza usumbufu wa kupata elimu.

"Ni kweli watoto wanabebeshwa mabegi makubwa yenye madaftari na vitabu, lakini wazazi na walezi nao wanalazima kulipa nauli kila siku, kama wangesoma karibu na nyumbani, gharama zingepungua," anasema Suzan.

Hatua ya kuongeza shule ingekwenda sambamba na kuboresha elimu, ili kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi na kuwavuta kusoma popote walipo, anaeleza.

"Ninaamini kuna jambo haliko sawa, hivyo, nirudie kwamba, kama serikali imeamua wanafunzi wasome shule za jirani iboreshe mazingira ya kufundisha na kujifunza," anasema.

Katibu wa Chama cha Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), Meshack Kapange anasema, kuna sababu zinazochangia hali hiyo.

Mojawapo anasema ni kuhama kwa familia kutoka eneo moja kwenda lingine kutafuta unafuu wa kodi au makazi ya kudumu.

Kapange anasema ni wale ambao hawajajenga nyumba wanalazimika kuhama makazi lakini wakiwabakiza watoto shuleni licha ya kwamba wanatembea kilometa nyingi kuzifikia.

"Lakini pia ubora wa shule nao unachangia wazazi kuwapeleka watoto kusoma kule wanakoona watafaulu hata kama ni mbali," anasema Kapange.

Katibu huyo anaongeza kuwa elimu ni kila kitu katika maisha na kwamba inatafutwa kwa gharama ikiwamo hiyo ya watoto kwenda kusoma mbali na nyumbani.

"Kwa ujumla sekta ya elimu ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi. Unapoona hali kama hiyo ya wanafunzi kutafuta elimu mbali, ujue kuna sehemu hakujakaa vizuri," anasema.

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Kumbe oksijeni duniani chanzo ni bahari si anga, mimea kama ilivyodhaniwa awali

MAMILIONI ya watu wanafahamu baada ya kufundishwa kuwa chanzo kikuu cha hewa ya oksijeni inayotumiwa duniani inatoka angani, pia inazalishwa na mimea inapotengeneza chakula na kiasi inapatikana kwenye ufa wa dunia.

Swali la ni nini chanzo kikuu cha oksijeni duniani linaendelea kutafitiwa. Ni mimea ipi huipa dunia oksijeni yote au anga? Jibu sasa linakuwa oksijeni duniani haitoki zaidi kwenye miti.

Badala yake, inatoka angani na ndiyo ambayo wanadamu wanaitegemea na kwamba kwa kiasi kikubwa inapatikana baharini, kwa mujibu wa Taasisi ya National Geographic.

Inaeleza kuwa, karibu asilimia 70 ya oksijeni katika angahewa hutoka kwenye mimea ya baharini na viumbe vinavyofanana na mimea.

Hivi karibuni wanasayansi hao, wamegundua oksijeni kwenye kina kirefu cha bahari, ikizalishwa na vipande vya mawe vilivyoko kwenye sakafu ya bahari.

Wanasema zaidi ya nusu ya oksijeni ambayo watu wanaitumia inatoka baharini. Lakini, kabla ya ugunduzi huo, ilieleweka kuwa inatengenezwa na mimea ya baharini, inayofikiwa na mwanga wa jua.

Katika kina cha kilomita tano ambapo hakuna mwanga wa jua unaoweza kupenya, oksijeni inapatikana ikizalishwa kwa wingi na vipande vya mawe.

Kwa haraka kampuni kadhaa za uchimbaji madini zinaeleza kuwa zina mipango ya kukusanya mawe haya, lakini wanasayansi wa baharini wanahofia kuyakusanya kwani kunaweza kuvuruga maisha ya viumbe wa baharini ambao wanategemea oksijeni inayozalishwa baharini.

"Niliona jambo hili kwa mara ya kwanza mwaka 2013, kiasi kikubwa cha oksijeni kinatoka kwenye sakafu ya bahari katika giza totoro," anaeleza mtafiti mkuu Prof. Andrew Sweetman.

Msomi huyo kutoka Chama cha Scotland cha Sayansi ya Bahari anaongeza. "Nilipuuza, kwa sababu nilikuwa nimefundishwa, oksijeni inapatikana tu kupitia kusanisi mwanga au nuru ya jua."

Yeye na wenzake walifanya utafiti katika eneo la kina kirefu cha bahari kati ya Hawaii na Mexico - sehemu ya sakafu ya bahari ambayo imefunikwa na vipande hivi vya mawe.

Anasema vipande hivi hujiunda vinapokusanyika na maganda magumu na taka nyingine, akisema ni mchakato unaochukua mamilioni ya miaka.



Timu ya kimataifa ya wanasayansi imegundua kwamba oksijeni inatoka kwenye mawe ya chuma yaliyoko chini ndani (sea bed) ya Bahari ya Pasifiki. **PICHA: MTANDAONI.**

> Ukiweka betri kwenye maji ya bahari, inaanza kutoa povu," anaeleza Prof. Sweetman na akiongeza kuwa, "Kwa sababu mkondo wa umeme kwenye maji ya bahari hugawanyika kuwa oksijeni na haidrojeni (ambayo ni mapovu).

Kwa sababu vipande hivyo vina madini ya 'lithiamu, kobalti na shaba', zote hizo zinahitajika kutengeneza betri. Kampuni nyingi za madini zinaunda teknolojia ya kuvikusanya na kuvileta juu duniani.

Ugunduzi uliochapishwa katika jarida la 'Nature Geoscience', unazua wasiwasi kuhusu hatari za uchimbaji wa mawe haya katika kina kirefu cha bahari.

Wanasayansi waligundua kuwa vipande hivyo vinaweza kutengeneza oksijeni kwa sababu vina sifa kama betri.

"Ukiweka betri kwenye maji ya bahari, inaanza kutoa povu," anaeleza Prof. Sweetman na akiongeza kuwa, "Kwa sababu mkondo wa umeme kwenye maji ya bahari hugawanyika kuwa oksijeni na haidrojeni (ambayo ni mapovu). Tunaamini vipande hivi, hufanya mchakato kama huo lakini kwa njia ya asili.

Watafiti katika maabara, walipima nguvu ya umeme kwenye vipande hivyo. Wakagundua kuwa umeme wake unakaribiana na umeme katika betri ya kawaida.

Hii inamaanisha, vipande vya mawe vilivyokaa chini ya bahari vinaweza kuzalisha umeme mwingi.

Watafiti wanafikiri mchakato wa kuzalisha oksijeni ambayo haihitaji mwanga wa jua unaweza kuwa unatokea kwenye sayari nyingine, na kuwa na mazingira yenye oksijeni ambako maisha yanawezekana.

Wasimamizi wa kitaifa wa masuala ya Bahari na Anga wa Marekani (NOAA), wameonya uchimbaji wa mawe hayo unaweza "kusababisha uharibifu wa maisha na makazi chini ya bahari."

Zaidi ya wanasayansi 800 wa baharini kutoka nchi 44 wametia saini onyo, linaloangazia hatari za kimazingira na kutaka kusitishwa kwa shughuli za uchimbaji wa mawe hayo.

Spishi mpya zinagunduliwa katika kina kirefu cha bahari kila siku na inaelezwa kuwa, wanajua zaidi kuhusu uso wa mwezi, zaidi ya wanavyojua kuhusu kina cha bahari.

Ugunduzi huu umefichua kwamba mawe yanayotoa oksijini yanasaidia maisha huko.

Prof. Murray Roberts, mwanabiolojia wa baharini kutoka Chuo Kikuu cha Edinburgh ni mmoja wa wanasayansi waliotia saini ombi la kuzuia uchimbaji huo baharini.

"Tayari kuna ushahidi mwingi kwamba uchimbaji wa mawe hayo kwenye kina kirefu cha bahari utaharibu mifumo ya ikolojia ambayo hatuielewi," anaiambia BBC.

"Kwa sababu mashamba haya yanafunika maeneo makubwa kama haya ya sayari yetu, itakuwa ni wazimu kufanya uchimbaji baharini huku tukijua kuwa ni chanzo kikubwa cha uzalishaji wa oksijeni."

Prof Sweetman anaongeza: "Sioni utafiti huu kama jambo ambalo litakomesha uchimbaji.

"Lakini tunahitaji kuchunguza kwa undani na tunahitaji kutumia taarifa hizi na taarifa tutakazokusanya siku zijazo, ikiwa tutataka kwenda kwenye kina kirefu cha bahari kuchimba kwa njia ambazo ni rafiki zaidi kwa mazingira."

Baadhi ya watafiti wa bahari wanaeleza kuwa kuna angalau mara tatu zaidi ya maisha kwenye sakafu ya bahari kuliko yale ya bahari iliyoko juu.

Na karibu theluthi mbili ya maisha hayo bado haijagunduliwa au kutambuliwa rasmi na binadamu.

Wanasema imejulikana tangu miaka ya 1960 kwamba aina mbalimbali za viumbe ziko juu sana kwenye kina kirefu cha bahari, na kwamba kuna anuwai nyingi lakini pia nasaba nyingi zisizojulikana na familia nyingi za viumbe zinazosubiri kugunduliwa.

Sakafu ya kina kirefu cha bahari inafunika zaidi ya nusu ya uso wa dunia lakini ni nyumbani kwa baadhi ya mifumo ya ikolojia ambayo haijasomwa sana, kulingana na utafiti huo.

Utafiti wa awali ulichanganua nasaba (DNA) iliyokusanywa kupitia safu ya maji, kutoka juu ya sakafu ya bahari kwa hivyo utafiti huu wa hivi karibuni unataka kukamilisha picha na kutoa mtazamo wa kimataifa wa viumbe hai ndani ya bahari.

Baadhi ya wanyama wanaoishi kwenye sakafu ya bahari wanaofahamika ni pamoja na dolfini, papa, ndege jamii ya pengwini na simba wa baharini.

**BBC SWAHILI**

TEKNOLOJIA

NA ENOCK CHARLES

# Mageuzi ya kielektroniki yawaunganisha wananchi,watoa huduma, vituo vya afya

MAGEUZI ya teknolojia yanayoendelea duniani, yameleta unafuu na urahisi katika sekta mbalimbali, afya ikiwa haijaachwa nyuma.

Kwa Tanzania mageuzi hayo yanakwenda sambamba na ongezeko la matumizi ya teknolojia ya kielektroniki kutengeneza mifumo inayotatua changamoto zinazowakabili wananchi wengi au makundi maalum.

Mkurugenzi wa Programu wa shirika la kiraia la Apotheker Health Access Initiative, Dk. Angel Dillip, anasisitiza umuhimu wa mageuzi ya teknolojia ya kidijitali kwa huduma za afya mijini na vijijini.

"Teknolojia ya kidijitali na matumizi yake katika huduma za afya ina uwezo wa kuboresha ufanisi, kupunguza gharama na kurahisisha kazi kwa watoa huduma wa afya ya msingi," anasema Dk. Dillip.

Anasema mwaka 2019, walisukumwa kuanzisha mpango wa kidijitali, Afya-Tek, kwa lengo la kusaidia juhudi na mipango ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa wanawake na utoaji wa elimu kwa vijana wa rika balehe.

Anasema mfumo huo pia unaunganisha maduka ya dawa binafsi, vituo vya afya na wahudumu wa afya ya jamii.

"Changamoto kubwa ambayo sisi tuliona ni kwamba hapakuwa na muunganiko kati ya watoa huduma wa afya ya jamii, maduka ya dawa na vituo vya afya pamoja na kwamba wote wapo katika jamii moja lakini hawaongei kitu kimoja," anasema Dk. Dillip.

"Tuliona ili hawa wote wafanye kazi pamoja wanahitaji kuunganishwa kwa mfumo mmoja wa kidijitali," anafafanua.

Anasema kupitia Afya-Tek, watoa huduma wa afya ya jamii 240 katika wilaya ya Kibaha wamewezeshwa kuwasajili watu wao ili waweze kuwatambua na kuwahudumia kirahisi katika mfumo wa kidijitali ambao umeunganishwa na vituo vya afya na maduka ya dawa.

Anatoa mfano kwamba Afya-Tek inaunda vitambulisho vya kipekee vya wagonjwa, vinavyowezesha utambulisho sahihi na upatikanaji wa haraka wa rekodi zao za afya.

"Teknolojia hii huongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za afya, kuhakikisha kuwa wagonjwa wanapata huduma kwa wakati na kwa uratibu."



Mama na mtoto huko Kibaha mkoani Pwani wakisajiliwa kidijitali na mtoa huduma wa afya ya jamii . **PICHA: AFYA-TEK**

Dk. Dillip anasema ili kufikia malengo ya kuwaunganisha watoa huduma za afya na wagonjwa, wanahamasisha viongozi wa mitaa na mafunzo kuwa watoa huduma.

"Afya-Tek imetoa mafunzo kwa karibu watu 500 wanaohudumia zaidi ya watu 255,000 na imeboresha sana huduma za afya. Mpango huo pia umerekodi

zaidi ya watu 100,000 kutembelea maduka ya dawa binafsi na kupata huduma kidijitali," anasema.

Mwenyekiti wa Maduka ya Dawa Binafsi Kibaha Mjini, Steven Bwire, anasema mpango wa kuhudumia wagonjwa kidijitali umesaidia kuwa na kumbukumbu zao sahihi na hivyo kuwapa huduma yenye mwendelezo mzuri akitolea mfano wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Anasema huduma hiyo imewezesha kuwa na kumbukumbu sahihi za mjamzito na hata anapoenda katika kituo cha afya inakuwa ni rahisi kuhudumiwa.

"Watu wengi wanapopata changamoto za kiafya kitu cha kwanza huwa wanakimbilia kwenye maduka ya dawa kupata huduma sasa mfumo huu unatusaidia kuwahudumia kirahisi na hata baadae anapoenda katika kituo cha afya inakuwa ni rahisi kuhudumiwa kwa kuzingatia kumbukumbu zake za nyuma," anasema Bwire.

Mariam Mbwana ni mama wa watoto watatu kutoka Visiga katika wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, anasema Afya-Tek imekuwa mkombozi kwake.

"Kabla ya Afya-Tek, kupata huduma ya afya ilikuwa vigumu, kwa mfumo wa kidijitali watoto wangu na mimi tunapata huduma kwa wakati unaofaa. Watoa huduma wa afya ya jamii daima wako kutuongoza, na hatuhitaji tena kuwa na wasiwasi kusubiri kwa muda mrefu katika kliniki," anasema Mariam.

Mbali na kutoa huduma rahisi kwa wajawazito na watoto, Afya-Tek imethibitisha kuwa ya manufaa hasa kwa vijana, ikiwafikia takribani vijana 28,000 na kuwapa taarifa na huduma muhimu za afya.



Mwenyekiti wa Watoa Huduma ya Afya ya Jamii, Ramadhan Shaban, anasema anafanyakazi hiyo kwa kujitolea kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Afya-Tek, vituo vya afya na maduka ya dawa.

Anasema mpango huo umesaidia vijana kupata elimu sahihi ya afya, magonjwa ya ngono na namna ya kuepukana na mimba katika umri mdogo.

Kwa wajawazito anasema wamepata urahisi wa kupata huduma haraka na hivyo kuongeza idadi ya mahudhurio yao ya kliniki.

"Sisi tuliwekeana malengo kwa kila mtoa huduma wa afya ya jamii kuhudumia wastani wa kaya 200 na makundi haya yote yanapatikana katika hizo kaya, imesaidia kupunguza vifo vya wajawazito na wengi kuona umuhimu wa kliniki," anasema Shaban.

"Tunasogeza elimu ya afya ya uzazi karibu na wananchi kwa hiyo hata kama kituo cha afya kipo mbali lakini kupitia sisi watoa huduma wa afya ya jamii mtu anaweza kupata huduma za awali kabla ya kufika kituo cha afya na vilevile tunakuwa kiunganishi kati ya vituo vya afya na wananchi kwa kuwa wakati mwingine wanatuelewa zaidi sisi tunaoishi nao kuliko wataalam wa afya," anasema Shaban.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Kibaha Mjini, Dk. Wilford Kondo, ambaye anasema pamekuwapo na ongezeko la wajawazito kuhudhuria kliniki kikamilifu na hatimaye kijifungulia hospitali badala ya nyumbani.

Anasema takwimu zinaonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko la wajawazito kupata huduma za uzazi hospitalini, kutoka asilimia 41 mwaka 2022 hadi asilimia 61 mwaka jana na hivyo kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na kupongeza mpango huo wa Afya-Tek wilayani humo.

"Tunahudumia wajawazito sasa unaweza kukuta mama damu imepungua hajapata lishe nzuri, sasa hawa wahudumu wa afya ngazi ya jamii kwa kuwa wanafanya kazi ngazi ya chini kabisa unakuta wanaibua hizo changamoto wanagundua matatizo haraka kutokana na elimu waliyopewa inarahisisha mama kwenda hospitali kwa wakati," anasema Dk. Kondo.

Akielezea kuhusu umuhimu wa watoa huduma wa afya ya jamii, anasema wanasaidia kufikisha elimu kwa umma na huduma za awali kule ambako wataalam wa afya wasingeweza kufika kirahisi na wanatumia lugha inayoeleweka kwa urahisi kuliko ile ya wataalamu wa afya.

"Sera ya nchi inaelekeza mama mjamzito awahi haraka kliniki mara tu anapojigundua ni mjamzito sasa kupitia hawa watoa huduma wa afya ya jamii hilo limefanikiwa kwa kiasi fulani," anaeleza.

Hata hivyo Dk. Kondo anaeleza kumekuwa na mimba za utotoni katika halmashauri hiyo na kwamba ripoti ya mwaka jana inaonesha kuwa Halmashauri hiyo ilirekodi mimba 637 na kuwaomba wadau mbalimbali kuendelea kuwaunga mkono katika juhudi za kupambana na tatizo hilo.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

JANGA HAKUNA AJIRA

# Wahitimu waandae cha kufanya baada ya kupata 'digirii' vyuoni

- Uje mkakati wa kupeleka wataalamu vijijini washiriki kuleta maendeleo

UHABA wa ajira ni mkubwa lakini kwa mataifa maskini ni tatizo linalozielemea serikali zote, kuliko kwenye mataifa yaliyoendelea.

Kwa mfano, Ulaya idadi ya watu ni ndogo huku wazee wakiwa wengi zaidi na kazi za kufanya ni nyingi pia.

Kinachojiri ni kazi nyingi lakini hakuna wakuzifanya. Na ili kutatua tatizo la nchi kukosa nguvu kazi, serikali huko Ulaya zinatoa ajira kwa wakimbizi au wahamiaji kutoka nchi zenye migogoro ikiwamo vita.

Mfano, ni rahisi kwa raia wa Ukraine kupata kazi Ulaya kutokana na vita na Urusi. Aidha. hata raia wa Ulaya Mashariki kama Belarus, Bulgaria, Cheki, Romania na Hangari nao wanaajiriwa kuziba pengo la kukosa nguvukazi.

Afrika shida ni kubwa kwa sababu ya umasikini na idadi kubwa ya watu hasa vijana. Kundi hili ni wengi zaidi na ajira ni chache mno, hivyo mamilioni hawana kazi wala hawawezi kujiajiri.

Takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), zinasema asilimia 70 ya watu Afrika Kusini ya Jangwa Sahara ni vijana walio na umri wa chini ya miaka 30.

UNFPA inasema kuwa idadi ya watu wa ukanda huo ni bilioni 1.2 hivyo vijana wanaweza kuwa zaidi milioni 840,000,000.

**VYANZO VYA AJIRA**


Msomi na mhubiri Askofu Victor Chisanga, Profesa mstaafu wa Chuo Kikuu cha Ardhi, anasema ukosefu wa ajira utapata tiba kwa kuzitaka taasisi za elimu ya juu kufanya utafiti kubaini wapi kuna fursa za kuajirika au kujiajiri ili kufundisha maeneo hayo zaidi.

Anasema wakati mwingine kufundisha wasomi wengi wasio na kazi tena wasioweza kujiajiri ni hasara kwa nchi kwa kuwa wengi wanasomeshwa kwa fedha za umma.

Anataka tatizo hilo limalizike kwa vyuo vikuu na vya kati kufanya kwanza utafiti, kutambua kada zenye ajira zaidi.

"Si hivyo tu pamoja na utafiti vijana wanapomaliza masomo wapate muda mwingine uwe mwaka au miezi sita kuandaa andiko la kile watakachofanya baada ya kupata shahada."

Profesa Chisanga mbobezi wa usanifu majengo 'architecture' anashauri msomi yeyote chuoni aandike atakachofanya baada ya shule.



Askofu Victor Chisanga

"Akiandaa andiko wahadhiri wafuatilie na kuona ubora wa kazi hizo, zile zitakazofaa zisimamiwe na kuendelezwa. Serikali iwakopeshe fedha za kuendeleza miradi hiyo ile inayoleta ajira kwa vijana wengi."

Anashauri kila kozi mwanachuo anayosoma aandae mikakati ya kujiajiri ili kupunguza tatizo linaloongezeka la kukosa kazi kwa wasomi wa vyuo vikuu na vya kati.

Msomi huyo anasema serikali ianzishe benki ya kutoa mikopo ya kufanikisha miradi hiyo, isimamie fedha hizo zirudishwe na kuendelea kunufaisha wanavyuo wengine.

**KUWAPELEKA VIJIJINI**

Tanzania nayo ina vijana mamilioni wasio na kazi lakini Profesa Victor Chisanga, anasema wanaajirika kupitia programu anayoiita 'kuajiri vijana wasio na ajira' kwa kupeleka maendeleo vijijini.

Anasema kazi itafanyika kwa kuainisha idadi ya vijiji wasomi wa kada zote na kuwapeleka vijijini ili waajiriwe kuanzia maofisa kilimo, wahandisi wa barabara, umeme, ujenzi, mipango miji, daktari mkuu/bingwa, wachumi na wataalamu wa ushirika.

"Tupeleke kila mtaalamu kijijini ili kufikisha maendeleo vijijini. Na wote wawe wasomi wenye 'degree' moja au zaidi.Tukisema matibabu yuko daktari bingwa au mkuu wa kijiji. Likiwa suala la elimu tunaye ofisa elimu wa kijiji. Tutaweza kuwaajiri vijana na wasomi wetu." Anasema Profesa Chisanga.

Anaongeza, mathalani kuna vijiji 12,000 wakiajiriwa wasomi 10 madaktari bingwa wa vijiji watakuwa 120,000, kadhalika wahandisi wa barabara na majengo na mipango waajiriwe.

"Ofisa kilimo atakuwa anachunguza ardhi, anashauri masuala ya mbolea, anafuatilia hali ya hewa, viuatilifu na kusimamia kilimo. Sekta hiyo itabadilika na kuimarika zaidi." Anaongeza.

Anasema kwenye ufugaji ofisa huyo na timu yake wanasimamia shughuli za ufugaji wa aina zote na kusimamia upatikanaji wa tija.

Anaamini kuwa iwapo wataalamu hao watapelekwa vijijini na kuajiriwa maendeleo yatapatikana na uhaba wa ajira unaweza kupunguzwa.

Pamoja na vijiji pia kwenye kata nako kuwe na wataalamu hao ili kusimamia na kushirikiana na wataalamu wa vijiji ili kutimiza malengo yanayowekwa ya kuleta maisha bora kwa wananchi.

**KUCHANGIA MAENDELEO**

Mbobezi huyo wa masuala ya usanifu anasema ili kuwapa vijana hao ajira ni lazima kuchangia mishahara akipendekeza kila mwanakijiji ahusike, waangalie idadi ya kaya na kukubaliana kiasi cha kutoa pengine Sh. 20,000 kwa mwaka.

Hata wale, walioko mijini wanaweza kuchangia kwa kutoa fedha hizo kwenye familia zao vijijini, ili zipatikane fedha za kutekeleza mradi huo na serikali ichangie.

"Takwimu zinatuambia kijiji kinaweza kuwa familia hata 800 na kila familia ina wastani wa watu watano hivyo tunakubalina kila familia ichangie pengine Sh. 20,000 au 15,000." Anashauri.

Wataalamu hao wanaweza kulipwa si chini ya Sh. 600,000 kwa mwezi sehemu ya mishahara hiyo ichangiwe na wanavijiji na halmashauri.

Anasema vijana hao wasomi wapelekwe vijiji kubadilisha sura ya nchi badala ya kuwaacha waendelee kuuza mafuta ya magari vituoni, kuendesha bajaji na boda au kuzurura mijini.

> Si hivyo tu pamoja na utafiti vijana wanapomaliza masomo wapate muda mwingine uwe mwaka au miezi sita kuandaa andiko la kile watakachofanya baada ya kupata shahada

**ULEVI**

Mwalimu huyo wa Injili, anagusia ukosefu wa ajira kwa vijana kuwa umechangia kuongezeka ulevi, akishauri ukomeshwe, kuwepo na sheria ya kufungua na kufunga baa kwa muda mfupi, lakini pia kuzuia uuzaji pombe kiholela na kuadhibu walevi kupindukia.

Serikali nayo inazungumzia suala la ukosefu wa ajira, kama Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa Pemba Januari, 2022 alisema tatizo la ajira ni kubwa na kwamba linalishughulikiwa .

"Serikali yenu, tunajua tatizo la ajira na tutajitahidi kutengeneza fursa mbalimbali ili vijana wapate ajira."

Vijana wengi wanaomba kazi kwa mfano umati ulipelekwa kufanyiwa usaili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa mwaka 2014, Idara ya Uhamiaji ilitangaza nafasi 70 za ajira na vijana zaidi ya 1,000 waliomba kazi na kusanyika kwenye uwanja huo, kusailiwa. Inamaanisha kuwa kati ya hao wengine 930 wameendelea kuishi bila kazi.

Kwa mujibu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, takribani vijana 1,000,000 wanahitimu kila mwaka kutoka taasisi mbalimbali za kielimu lakini kazi za ajira zinazopatikana kwenye sekta ya umma na binafsi hazizidi 300,000.

Hivi karibuni Rais Samia alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete kufanyakazi ili vijana wapate kazi.

Anamtaka kazi yake kubwa iwe kuratibu vijana wapate ajira na kuwe na uzalishaji wa kazi katika sekta nyingine mfano, kilimo, madini na uvuvi.



# DC apiga 'stop' mikokoteni ya ng'ombe barabarani

**Na Paul Mabeja, KONGWA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Mayeka Simon amepiga marufuku mikokoteni inayokokotwa na ng'ombe kutembea barabarani zaidi ya saa moja jioni, kwamba kinyume na hapo wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua ili kuwa na usalama barabarani.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2023/24 uliojumuisha wadau mbalimbali

Katika kikao hicho alitoa hati za pongezi kwa kata na vituo vya kutolea huduma za afya na wadau wa lishe waliofanya vizuri katika utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha mwaka 2023/2024.

Waliopata hati hizo ni Kata za Matongoro, Sagara na Mamlaka ya Mji Mdogo Kongwa, Hospitali ya Wilaya Kongwa, Kituo cha Afya Mlali na Ugogoni na mdau kutoka Shirika la CUAMM Doctors with Africa.

Mayeka aliwaagiza watendaji kusimamia upandaji wa miti ya matunda katika taasisi zote, ofisi za watendaji wa vijiji na kata uwepo wa vyoo vizuri vinavyotumika katika kila kaya na usafi wa mazingira kila Jumamosi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kongwa, Dk. Omary Nkullo aliwataka maofisa ustawi wa jamii kuongeza nguvu ya ushawishi katika kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya lishe ili kuepukana na tatizo la utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Ofisa Lishe wa Wilaya ya Kongwa, Maria Haule alisema katika kupambana na utapiamlo wilaya imefanikiwa kununua mashine nne za kuongeza virutubisho shuleni, kuongeza idadi ya wanafunzi wanaokula chakula shuleni kwa kipindi cha Januari hadi Machi kutoka wanafunzi 99,009 kati ya 126,936 wanapata chakula shuleni.

Alisema fedha zilizopangwa kutumika katika kutekeleza afua za lishe ni Sh. milioni 27.183 sawa na asilimia 91.83 ya fedha zilizotumika kwa ajili ya chakula shuleni na kutekeleza Siku ya Afya ya Lishe Vijijini.

Akizungumza kwa niaba ya Ofisa Kilimo wa Wilaya, Josiah Chikoka alisema amepokea na kufanyia kazi ushauri aliopewa na Mkuu wa Wilaya wa kushirikiana na taasisi mbalimbali kuzalisha kwa wingi mazao ya lishe ikiwemo matunda, mboga na viazi lishe.

## Jamii yatakiwa kurudi katika misingi ya utanzania

**Na Gloria Maganza,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu ameiasa jamii kurudi katika misingi ya utanzania na kuhakikisha kuwa suala la mmomonyoko wa maadili linapewa kipaumbele kuanzia ngazi ya familia.

Amesema lengo ni kizazi cha sasa na cha baadaye kiendelee kubaki salama na kujenga taifa lenye watu waliostaarabika

Alitoa nasaha hizo wakati wa mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi ya Martin Luther iliyopo jijini hapa.

Gugu alisema kwa sasa nchi inakabiliwa na janga la mmomonyoko wa maadili ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri jamii.

"Nitumie fursa hii kuiasa jamii kwa ujumla kurudi katika misingi yetu ya kitanzania na kuhakikisha kuwa suala hili la mmomonyoko wa maadili tunalipa kipaumbele ili watoto wetu waendelee kubaki salama na hatimaye kujenga taifa lenye watu wastaarabu" alisema Gugu.

Aidha, aliitaka shule hiyo kuzingatia misingi muhimu iliyowekwa na serikali katika kuwaandaa watoto ikiwa ni pamoja na kuwajenga wanafunzi wenye uwezo wa kuwasiliana kwa lugha fasaha kama lugha ya taifa (Kiswahili) lugha za kigeni ikiwemo Kiingereza, lugha ya alama, breli na lugha ya mguso.

Awali Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Gilbert Nhuguti alisema wanafunzi 195 wakiwemo wasichana 102 na wavulana 93 ndiyo wanaotarajiwa kuhitimu.



Aliyekuwa Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Asma Karama (kulia) akimvalisha Joho la Unaibu Meya Fadhili Chibago (kushoto) baada ya kuchaguliwa kuwa Naibu Meya wa Jiji la Dodoma kwenye kikao cha Baraza kilichofanyika katika Jiji la Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Vijana waonywa unywaji pombe kupita kiasi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MBUNGE wa Singida Mjini, Mussa Sima amewataka vijana kuepuka unywaji wa pombe kupita kiasi.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi katika Soko Kuu la Singida baada ya mmoja wa wananchi kuomba serikali itafute namna ya kukomesha vitendo vya unywaji wa pombe kali, kwani vijana wengi wameathirika na kukosa nguvu.

Sima alisema pombe zinazowaumiza vijana hasa ni zile kali ambapo baadhi wanakunywa bila kula chakula na kuwaomba kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi hali inayosababisha washindwe kufanya shughuli za maendeleo.

"Nataka nitoe rai kwa vijana wenzangu tunahitaji nguvu kazi yenu, nguvu kazi yenu ndiyo maendeleo ya taifa hili, hivyo hata kama unahitaji kunywa pombe ujue kuwa wewe ndiyo nguvu kazi ya taifa hili unayetegemewa," alisema.

Akizungumza suala la wafanyabiashara wanaofanyia biashara katikati ya barabara katika Soko Kuu la Singida, alisema muda wa kuanza biashara hiyo ulioweka na serikali uzingatiwe na kwamba yeye hawezi kwenda kinyume na maamuzi yaliyotolewa na Serikali ya Wilaya ya Singida.

Kuhusu ombi la wafanyabiashra hao kwamba muda huo unawabana, wanashindwa kufanya biashara kwa muda mrefu na hasa ikizingatia wengine wanakaa mbali na soko hilo, Sima aliwahidi kuliwasilisha kwa Kamati ya Usalama ya Wilaya ili kuangalia kama wanaweza kuongeza muda kwamba waanze kufanya biashara saa 11:00 jioni.

Alisema amekuwa akijitahidi kuboresha miundombinu ya soko hilo na kuahidi kwamba ataendelea kufanya hivyo kwa kutoa pesa ili mazingira ya soko yaendelee kuwa ya kuvutia.

Aidha, aliwataka wananchi kujiunga na bima ya afya iliyoboresha ili waweze kupata huduma za afya kwa urahisi.

# 20 wafanyiwa upasuaji wa ngirimaji, tezi dume bure

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA kutibu magonjwa ya ngirimaji, saratani ya tezi dume na henia, wagonjwa zaidi ya 20 wamepatiwa matibabu ya upasuaji bure katika Taasisi ya Shree Jalaram Seva Mandal.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Kishor Modi alisema wamekuwa wakitoa huduma hiyo kwa zaidi ya miaka 21.

Pamoja na mambo mengine, alikabidhi fomu 20 kwa wagonjwa ambao wapo tayari kufanyiwa upasuaji wa magonjwa hayo.

Alisema ni kawaida kwa taasisi yao kusaidia makundi mbalimbali yakiwemo wasiojiweza na watu wenye ulemavu kwa kuwapatia msaada huo wa ufanyiwaji wa upasuaji katika magonjwa hayo.

Alisema tayari wamefanikiwa kuwasaidia Watanzania mbalimbali katika kufanya upasuaji huo na wengine kuwapatia vifaa saidizi kama viti mwendo, magongo ya kutembea, baiskeli za watu wenye ulemavu pamoja na kusaidia vyakula kwenye vituo mbalimbali vya watoto yatima na wasiojiweza pamoja na kuwasomesha.

"Taasisi yetu ipo kwa ajili ya kusaidia watu wowote na kugharamia baadhi ya vitu, hivyo wagonjwa kama hawa wa ngirimaji, tezi dume pamoja na henia wanakuja wenyewe hapa au kutumia mitandao yetu ya kijamii na kuomba kusaidiwa, hivyo tunawajazia fomu na kuwapeleka hospitali kwaajili ya matibabu ya upasuaji," alisema.

Katibu wa Afya kutoka Hospitali ya Hafford, Shafii Hemed, alisema takribani miaka 21 sasa wamekuwa wakitoa huduma bure za matibabu kwa makundi hayo.

Alisema magonjwa ya ngirimaji, tezi dume pamoja na henia yamekuwa yanaongezeka kwa kasi kutokana na watu kutozingatia chanjo na kampeni mbalimbali zinazoendeshwa na wizara husika.

"Gharama za matibabu kwa haya magonjwa ni kuanzia Sh. 400,000 hadi 500,000 kwa upasuaji mmoja, hivyo kama mgonjwa wa kipato cha chini ni ngumu kupata matibabu haya endapo hatasaidiwa," alisema Hemed.

Mwakilishi wa kituo cha watoto yatima cha Chamazi Group, Haruna Mtandika, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuendelea kusaidia makundi mbalimbali ikiwemo ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mmoja wa wagonjwa waliopata matibabu mkoani Morogoro, Alfat Kaunda aliishukuru taasisi hiyo kwa kusaidia kundi kubwa la Watanzania katika kupata matibabu hasa kundi lenye uchumi wa chini.



# Wadudu wasiofahamika washambulia pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADUDU wasiofahamika wameanza kushambulia pareto katika baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, hali ambayo inadaiwa kushusha ubora wa zao hilo na kuhatarisha uchumi wa wakulima wa maeneo hayo.

Kutokana na tatizo hilo, wakulima wa maeneo hayo wameiomba serikali kuwasaidia kupata dawa za kuua wadudu hao wakidai kuwa mpaka sasa hawajui dawa inayoweza kuwadhibiti.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya siku ya pareto ambayo yalifanyika katika Kijiji cha Jojo kilichopo Kata ya Santiliya, ambapo walisema haijawahi kutokea tangu walipoanza kuzalisha zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Daniel Solomon alisema wadudu hao wanashambulia maua ya zao hilo na kusababisha lianze kusinyaa na kukauka kabla halijakomaa na hivyo kusababisha mavuno kushuka.

Alisema wakati mwingine wanashambulia maua hayo yakiwa yanaanza kuchanua na kwamba ikitokea mkulima akachuma maua yaliyoshambuliwa na wadudu hao yanakuwa machafu na hivyo kuharibu soko.

"Sisi kama wakulima hatuna utaalamu wa kukabiliana na wadudu hawa, kwahiyo tunaiomba serikali itusaidie kupata dawa ambayo tutaitumia kuwadhibiti wadudu hawa, mpaka sasa hatuelewi cha kufanya," alisema Solomon.

Naye Saimon Mwampamba alisema wao miaka yote walikuwa wanaamini kwamba pareto haiwezi kushambuliwa na wadudu kwa sababu yenyewe ni sumu na inatumika kutengeneza viuatilifu ambavyo ni sumu ya kuua wadudu.

Alisema tangu walipoanza kulima zao hilo ni mara ya kwanza kushuhudia wadudu kushambulia zao hilo, huku akidai kuwa kuna uwezekano tatizo hilo linasababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, watafiti wa taasisi mbalimbali za serikali wameshaanza kufanya utafiti ili kuwabaini wadudu hao na njia ya kuwakabili.

Alisema mpaka sasa watafiti kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya na maofisa Mamlaka ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) wameshaanza kufanya utafiti ili kuwabaini wadudu hao.

"Lakini pia TARI wametuhakikishia kwamba wanaendelea na utafiti wa mbegu ambazo zitakuwa na uwezo wa kukinzana na wadudu hawa pamoja na magonjwa ambayo yanaweza yakajitokeza, kwahiyo nawaomba wakulima wasiwe na wasiwasi," alisema Mapunda.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Mohamed Fakii aliwataka wakulima kushirikiana na wataalamu wanaofanya utafiti ili suluhu ya kudumu ipatikane haraka.

## Tafrani yazuka madai Mamlaka Mji Kyela kuvunjwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

VIONGOZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela mkoani Mbeya, wamelilalamikia Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kuanzisha mchakato wa kuifuta mamlaka hiyo bila kuwashirikisha, wakidai kuwa mchakato huo umeibua sintofahamu kwa wananchi.

Walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki walipozungumza na wandishi wa habari ambapo walisema mamlaka hiyo ilianzishwa ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo, Emmanuel Bongo alisema kuna vikao mbalimbali vya baraza la madiwani ambavyo vimekuwa vikifanyika kwa lengo la kuvunja mamlaka hiyo jambo ambalo alisema siyo halali.

Alisema baada ya taarifa kusambaa kwamba mamlaka hiyo inavunjwa, wananchi wameanza kulalamika wakiomba mchakato huo usitishwe ili waendelee kuhudumiwa na mamlaka.

Alisema kila mwaka wamekuwa wakifikia lengo la ukusanyaji wa mapato lakini halmashauri inataka kuivunja mamlaka hiyo kwa kigezo kuwa inaongeza gharama za uendeshaji kwa kutegemea mapato ya halmashauri.

Baadhi ya wananchi wa mamlaka hiyo waliiomba serikali kuwasaidia kusitisha mchakato wa kuivunja mamlaka hiyo wakidai kuwa utawarudisha nyuma kimaendeleo.

Mmoja wa wananchi hao, Eliada Mwansansu alisema baada ya mji huo kuanzishwa kuna shughuli ambazo huwa zinafanyika kwenye vijiji walizuiliwa kuzifanya na hivyo kuwarejesha kwenye vijiji itakuwa vigumu.

Alisema kitendo cha kutaka kuivunja mamlaka hiyo kitawasababishia usumbufu wa kufuata huduma za jamii katika Halmashauri ya Kyela ambako ni mbali.

Naye Anyelwike Mwasipu, alisema kitendo cha kuifuta mamlaka hiyo kitaonyesha kama serikali ilikuwa inafanya majaribio katika kuleta huduma kwa wananchi jambo ambalo siyo sahihi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono alisema kwa sasa wanachosubiri ni maamuzi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambako alisema walishawasilisha.



Baadhi ya wananchi wa kutoka katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Mbeya na Songwe wakifurahia katika ufukwe wa Matema uliopo ndani ya Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waziri Maliasili ahimiza utunzaji mazingira

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana amewataka wananchi kuacha kuharibu mazingira na badala yake wajenge utamaduni wa kuyahifadhi ili kupunguza tatizo la mabadiliko ya tabia nchi.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Njombe, ambalo liliambatana na uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025.

Dk. Chana alisema ipo haja ya jamii kukumbushwa umuhimu wa kutunza mazingira pamoja na kuacha tabia ya kukata miti ovyo hali itakayosaidia kupata mvua nyingi na chakula cha kutosha.

"Tupande miti kwa wingi na tukishapanda tutakuwa na uhakika wa kupata mvua, kutakuwa hakuna jangwa vilevile tutapata chakula," alisema Dk. Chana.

Vile vile, Dk. Chana alitumia fursa hiyo kuwakaribisha watalii mkoani humo kwa sababu ya uwepo wa vivutio vya utalii ikiwemo Hifadhi ya Taifa Kitulo na Hifadhi ya Wanyapori ya Mpanga Kipengele.

Hata hivyo alisema wizara hiyo imepiga hatua kubwa baada ya uwekezaji wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutengeneza filamu ya The Royal Tour na kutumia Lugha ya Kiswahili katika mikutano mbalimbali ya kimataifa.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Julius Peter aliwataka wanawake wa chama hicho kuwa tayari na kujindaa kushiriki kuhamasisha kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura.

Pia kufanya maandalizi ya kuhakikisha ushindi unapatikana kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao unatarajia kufanyika Novemba mwaka huu.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Mkoa wa Njombe, Scolastica Kevela aliitaka jamii mkoani humo kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.





# ACT yaja juu tozo miundombinu ya umeme kupandishwa kinyemela

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema kitendo cha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupandisha tozo ya miundombinu ya umeme visiwani hapa bila kutangaza na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ni kinyume na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu wakati akihutubia wananchi katika Kijiji cha Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja baada ya tozo hiyo kupandishwa kutoka asilimia mbili hadi saba .

Jussa, alisema kwa mujibu wa katiba, Baraza la Wawakilishi ndiyo lenye mamlaka ya kuidhinisha mabadiliko ya tozo za malipo ya kodi.

Alisema tozo ya huduma hiyo haijapitishwa na badala yake wananchi wameanza kutozwa kimya kimya na kuwaongezea ukali wa maisha.

"Siku za karibuni wamependisha bei ya umeme bila ya kututangazia, tizameni risiti mnazonunua umeme mnapata uniti ngapi?, mnajua nini kilichopo kuna kodi ya miundombinu ambayo iliyokuwa ikikatwa asilimia mbili kila unaponunua umeme, lakini sasa unakatwa asilimia saba," alisema Jussa.

Vilevile alisema kwa mujibu w a katiba ya Zanzibar, mwenye mamlaka wa kuweka, kuongeza au kupunguza kodi ni Baraza la Wawakilishi ambalo ni chombo cha kuwakilisha wananchi.

Jussa, alisema tozo iliyoongezwa ni sawa na ongezeko la asilimia 250, hivyo kuwa mzigo kwa wananchi kwa vile umeme ni nguzo ya maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

Akizungumzia kukwama kwa mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, barabara ya Mkoani Chake-chake, Tunguu- Makunduchi na Kisaun- Fumba, alidai mradi huo umekumbwa na ufisadi kwa maslahi binafsi.

Alitaka uchunguzi ufanyike kwa kuwa mradi huo ni muhimu katika kuimarisha sekta ya uchukuzi na usafirishaji visiwani hapa.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Nassor Ahmed Mazrui, alisema amelelewa kisiasa na mwanasiasa mkongwe marehemu Maalim Seif Sharif Hamad na hawezi kwenda kinyume na malezi yake na misingi aliyokuwa akiitetea.

Mazrui ambaye pia ni waziri wa afya, alisema Maalim Seif aliwafundisha siasa na kuwausia umuhimu wa Zanzibar kuwa na mamlaka kamili na ndio ajenda ya chama hicho ili iweze kufunguka kiuchumi.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Mansour Yussuf Himid, alisema bado Zanzibar imeendelea kuwekewa vikwazo vya utafiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi licha ya kuwa rasilimali hiyo ni ya visiwa hivyo.



Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo Nassor Mazrui akishangiliwa na wafuasi wa chama hicho baada ya kufika katika mkutano wa hadhara wa chama hicho ambao umefanyika Matamwe Kijini Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mazrui pia ni Waziri wa Afya Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi waonya kauli za viongozi wa siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar, limewaonya baadhi ya wanasiasa kuacha kutoa kauli zitakazosababisha chuki, uhasama na vurugu katika jamii visiwani hapa.

Onyo hilo lilitolewa jana na Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis.

Wakati akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya jeshi hilo visiwani hapa.

Kamishna Khamis, alisema kuwa jeshi hilo linatambua kuwa uhuru wa kuzungumza ni haki ya demokrasia nchini na ni lazima itekeleze uwajibikaji kwa kudumisha amani, utulivu na utawala wa sheria.

Alisema jeshi hilo linaheshimu haki za viongozi wa siasa ambavyo vyama vyao havijaunda serikali, kuikosoa mapungufu yake na kushawishi wafuasi kwa njia halali kuleta mageuzi kwa utaratibu uliowekwa kisheria kwa maslahi ya nchi na watu wake.

Kamishna huyo, alisema katika mikutano ya siasa inayoendelea visiwani hapa, ameshuhudia na kusikia baadhi ya viongozi wakitoa matamshi ya uchochezi kwa lengo la kuleta chuki, dharau kwa mamlaka halali na kuchochea hasira na uhasama.

Alionya kuwa hali hiyo inaweza kusababisha vurugu katika jamii kwa kisingizio cha haki ya uhuru wa kujieleza.

Alisema pia wapo viongozi wa siasa wamesikika wakisifia au kushabikia vitendo vya uvunjifu wa amani, kuhamasisha wafuasi wao kuchukua sheria mkononi kama njia ya kujibu maneno ya uchochezi, kejeli na kuingilia faragha.

Kamishna huyo, alisema vitendo hivyo vinazoofisha mshikamano wa jamii na utawala wa sheria nchini.

Aliwataka viongozi wa siasa kutumia uhuru wao kujieleza kwa sababu ndio msingi wa demokrasi na kutambua wanawajibika kisheria kwa wanachama, wafuasi wao na jamii bila ya kuathiri haki ya mtu mwingine.

Alisema viongozi hao wenye nia njema na nchi wanaweza kuingia kwenye mijadala mikali ya siasa yenye nia ya kuijenga nchi na kukosoana bila ya kutumia matamshi yenye kuibua hisia na yenye kuhatarisha amani na utulivu nchini.

Kamishna huyo, aliwaagiza makamanda wa polisi wa mikoa yote ya Zanzibar kusimamia sheria dhidi ya uchochezi

wenye mwelekeo wa kusababisha ghasia, matamshi ya chuki au dharau kwa serikali, kuhamasisha watu kuleta mageuzi kwa njia isiyo halali, watu waende kinyume na utawala wa sheria, kukuza hisia za nia mbaya na chuki baina ya watu wa Zanzibar na uchochezi.

Alisema kwa kutumia mpango wa ushirikishaji wa jamii na washikirikiane na wadau wa amani, watumie fursa hizo kuelimisha umma kuhusu hatari ya maneno ya uchochezi, uzushi, dharau na kejeli dhidi ya watu binafsi na serikali kwa usalama wa nchi.

Aliwataka waelimishe jamii umuhimu wa kuendesha mikutano ya siasa kwa njia ya kistarabu, heshima na kuheshimiana.

Aliwataka waendelee kushirikiana na viongozi wa serikali, vyama vya siasa, jamii na mashirika kujenga maelewano na kupunguza mivutano ili kudumisha amani.

Kamishna Hamad aliwataka wananchi wakatae ushawishi wa kutumika, kuchochea, kuhamasisha au kuanzisha vitendo vya uvunjifu wa amani.

## Mbunge awakumbusha viongozi majimbo wajibu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Jimbo la Mahonda Abdallah Ali Mwinyi amesema ni wajibu wa viongozi wa majimbo kuisaidia serikali kupeleka maendeleo maeneo ambayo bado hayajafikiwa na miradi ya maendeleo ili kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Aliyasema hayo katika hafla ya ugawaji wa mitungi ya gesi 150 kwa mamalishe na babalishe, vifaa vya maji kwa wakazi wa Shehiya ya Kilombero, mabati kwa madrasa ya Matetema na Mahonda, ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi CCM kuanzia mwaka 2020 hadi 2025, iliyofanyika Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema anatambua kuwa katika jimbo hilo kuna changamoto zinawakabili wananchi na serikali imekuwa ikijitahidi kufanya kila juhudi kukabiliana nazo na kuwaletea maendeleo ili waishi katika mazingira bora.

Alisema ni wajibu wao kama viongozi wa majimbo kuhakikisha sehemu ambazo hawajazifikia kuwasaidia na kupata maendeleo.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na maji safi na salama, afya, elimu na barabara za ndani.

Akizungumzia mamalishe na babalishe, alisema ni kundi ambalo linahitaji kupata usaidizi ili kuendesha shughuli zao na kujiajiri wenyewe.

Aliwataka kungana na kujisajili ili ofisi yake ihakikishe wanawapatia mikopo kupambana na tatizo la ajira nchini.

Alisema akiwa kama kiongozi amekuwa akitatua baadhi changamoto ndani ya jimbo hilo kwa mafufaa ya wananchi wake.

Akizungumzia kuhusu ajira, alisema hilo ni tatizo kubwa duniani na kwamba wajibu wao washirikiane ili waweze kujiajiri.

Awali Katibu wa Jimbo hilo, Simba Haji Mcha, alimshukuru i mbunge huyo kwa kutoa msaada huo kuhakikisha anatekeleza kwa vitendo ilani ya chama hicho ambayo alikabidhiwa na kuifanyia kazi.

Aliwataka mamalishe na babalishe hao waendelee na moyo walio nao wa kuimarisha maendeleo yao katika jimbo.

Katibu wa Vijana CCM Wilaya ya Kaskazini B, Ashura Mohammed Ali, aliwataka kutumia kwa uangalifu vifaa hivyo, vinginevyo vitawaangamiza.

Kwa upande wao, mamalishe na babalishe hao waliomba kupatiwa mafunzo ya matumizi ya majiko hayo ili kuepuka hasara.

Pia waliomba kupatiwa hati za usajili kwa vikundi vyao ili waweze kujiendeleza na kupata mikopo haraka kutoka serikalini na taasisi za fedha nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ADELINA LAMECK MELIKZEDECK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1278-0003** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MBEZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/25595/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALMA EMMANUEL TENGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S4565/0528/2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **GILI HIGH SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **PHQ/MOR/MOR/26881/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THERESIA EMMANUEL MASSAWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 746 DMW.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/174678/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LILIAN FIDELIS NJAU**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 950 ASY** CHASSIS NO **TDO1W-208868** NA ENGINE **NO G16A1590CC** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/KIL/MOS/ 19102/2024**

## MLAU SECURITY COMPANY LTD.

Karibuni huduma bora ya uhakika ya ulinzi na usalama wako na mali zako. Tuna askari wenye mafunzo, silaha na vitendea kazi vya kisasa, gharama ni mapatano na mteja.

Tunalinda ofisi, nyumbani, Kanisani, Hotel, lodge, baa, car wash, parking store, maghala, maduka, masoko, shule, taasisi binafsi, sherehe, mikutano, kusindikiza mali au misafara (escort) pamoja ulinzi binafsi (Body guard).

Tuna nafasi za kazi ya uaskari, wanaohitaji wawe na mafunzo na vyeti,waliofanya kazi ya uaskari,wote wawe na wadhamini wawili na barua za utambulisho zenye picha zao.

**Wasiliana nasi kupitia**
**S.L.P.841 Tabora (H.Q)**
**simu:0688 310 560 , 0783 011 898 au fika ofisini Boma Road jirani na V.O.T FM Redio mjini Tabora.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BERA ANDREW KARUMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MERCEDES BENZ** yenye usajili namba **T 352 CVQ,** CHASSIS NAMBA: **WDC2030462R1160648** na ENGINE NAMBA: **271EAA0648.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DOD/DOD/35373/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**(Rule 13subordinate courts civil procedure summons and pleadings)**
**(Rules 1951 G.N. No. 292/55 Cap 2/64)**

**IN THE DISTRICT COURT OF KIGOMA DISTRICT AT KIGOMA**

**Civil appeal NO 6413/2024 (criminal case No.......of.........**

**GEORGE MASIMBA ........................................APPELLANT**

**Versus**

**MGITYA .N. CHACHA ..................................RESPONDENT**

**TO: MGITYA CHACHA**

**TAKE NOTICE THAT** the hearing of the above suit has been set down for HEARING on 26 AUGUST 2024

You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the documents upon which you intend to rely/reply insupport of your case.

AUGUST 2024 ON 26

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI** **Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Shauri la madai/ Ndoa Na 1345/2024**

**Jina la Mdai........................................HELLEN .E. LYIMO**

**Jina la Mdaiwa.....................SIGFRID .S. ...MWALUTAMBI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa SIGFRID .S. MWALUTAMBI**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 27 mwezi 08 mwaka 2024 saa 8:00 asubuhi mbele ya Mh. KINGU kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini , mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama leo tarehe 14 mwezi 08 mwaka 2024

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi la Ukraine lavunja madaraja Russia

**KYIV,** Ukraine

UKRAINE imesema imeliharibu daraja muhimu kwenye mkoa wa Kursk nchini Russia na kulishambulia jingine la karibu na hapo, chini ya wiki mbili tangu ianze uvamizi wake ulioziharibu kabisa njia za kusambazia vifaa vya kivita vya taifa hilo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Russia, hatua hiyo inaingilia moja kwa moja uwezo wa jeshi la taifa hilo hasimu kufikisha vifaa na bidhaa linazohitaji kukabiliana na uvamizi huo wa Ukraine.

Ilielezwa kuwa bado jeshi la Russia linaweza kutumia vivuko na madaraja madogo madogo kwenye eneo hilo. Huku Mkuu wa jeshi la anga la Ukraine, Luteni Mykola Oleshchuk, akichapisha video ya mashambulizi ya anga yaliyolisambaratisha daraja hilo vipande viwili.

Kwa mujibu wa Gavana wa jimbo hilo, Alexei Smirnov, chini ya siku mbili baada ya hapo, vikosi vya jeshi la Ukraine vilivunja daraja jingine nchini Russia. Na kwamba kufikia asubuhi ya Agosti 18, mwaka huu hakukuwa na taarifa yoyote rasmi juu ya lilipo daraja la pili lililoshambuliwa.

Chaneli za mtandao wa Telegram zilidai kwamba daraja hilo lilikuwa kwenye kijiji cha Zvannoe kando kidogo ya mji wa Seim. Huku mtandao wa Mash wa Russia, ukieleza kuwa mashambulizi hayo yamelibakishia eneo hilo daraja moja tu kwa sasa.

Shirika la habari la AP halikuweza kuthibitisha madai hayo mara moja, lakini endapo yakithibitishwa, basi mashambulizi ya Ukraine yatakuwa yanazidi kurejesha nyuma juhudi za vikosi vya Russia kuukomboa mkoa wa Kursk na kuwahamisha raia.

Hata hivyo, Kyiv imekuwa haisemi mengi kuhusu mipango na malengo ya uvamizi wake huo wa kushtukiza, yakiwa mashambulizi ya kwanza makubwa kabisa dhidi ya Russia tangu kumalizika kwa Vita vya Pili vya Dunia, na ambayo yaliishangaza Kremlin na kushuhudia vijiji kadhaa na mamia ya wafungwa wakiangukia mikononi mwa Ukraine.

Vile vile, ilielezwa kuwa Jeshi la Ukraine limeingia ndani kabisa ya mkoa wa Kursk wakipitia maeneo mbalimbali, huku wakikumbana na upinzani mdogo kabisa na kusababisha mtafaruku na fadhaa miongoni mwa raia.

Kamanda wa jeshi la Ukraine, Jenerali Oleksandr Syrskyi, alidai wiki iliyopita kwamba vikosi vyake sasa vinadhibiti eneo lenye ukubwa wa kilomita 1,000 za mraba ndani ya mkoa wa Kursk.

**DW**

# Kipindupindu chaua watu 22 nchini Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

SERIKALI ya nchini Sudan imesema takribani watu 22 wamefariki kutokana na ugonjwa wa kipindupindu huku visa 354 vikiripotiwa wakati vita ya wenyewe kwa wenyewe ikiendelea.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Afya, Haitham Mohamed Ibrahim, baada ya kufanyika mkutano na Naibu Kiongozi wa Baraza Kuu la Sudan, Malik Agar.

Waziri huyo alisema juhudi zinaendelea ili kuhakikisha upatikanaji wa maji salama ya kunywa, kukabiliana na waenezaji wa magonjwa, na kushirikiana na jumuiya ya kimataifa kupata chanjo ya kipindupindu.

Pia, alitoa wito kwa mamlaka za mitaa katika majimbo ya Sudan kuongeza juhudi zao za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Aidha, ilielezwa kuwa Sudan imetumbukia katika mzozo tangu Aprili 2023 huku kukiwa na mapigano kati ya jeshi na kundi la wanamgambo la Msaada wa Haraka (RFS).

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa (UN), zaidi ya watu 18,800 wamekufa katika vita hiyo, karibu milioni 10 wamekimbia makazi yao na zaidi ya milioni 25 wanahitaji msaada wa kibinadamu.

**TRT**




Kaimu Mratibu wa Huduma za Dharura wa Umoja wa Mataifa, Joyce Msuya, akizungumza kwenye Baraza la Usalama la Umoja huo, jana. **PICHA: MTANDAO**.

# OCHA: Watoa huduma za kiutu 280 wameuawa

**NEW YORK,** Marekani

OFISI ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa (OCHA) imesema wafanyakazi 280 wameuawa kwenye mataifa 33 katika mwaka 2023, huku ikitahadharisha kwamba huenda mwaka huu hali ikawa mbaya zaidi.

Hayo yalibainishwa jana wakati dunia ikiadhimisha siku ya huduma za kibinadamu huku Umoja wa Mataifa ukisema mauaji ya 2023 yalivunja rekodi, na kwamba hiyo ni ongezeko la asilimia 137 na zaidi ya mara mbili ya vile hali ilivyokuwa mwaka 2022, ambako wafanyakazi 118 waliouawa.

Kaimu Mratibu wa Huduma za Dharura wa Umoja wa Mataifa, Joyce Msuya, alisema vifo vingi zaidi vya 2023 vilitokea kwenye Ukanda wa Gaza katika miezi mitatu ya mwanzo ya mashambulizi ya Israel kwenye ukanda huo yaliyoanza mwezi Oktoba.

"Hali ya kufanya mashambulizi dhidi ya wafanyakazi wa misaada kuwa jambo la kawaida na ukosefu wa uwajibikaji ni mambo yasiyokubalika, yasiyoingia akilini na yenye madhara makubwa kwa operesheni za misaada popote yanapotokea.

"Wenye madaraka lazima wachukuwe hatua za haraka kukomesha mashambulizi dhidi ya raia na hali ya wahalifu kutokuchukuliwa hatua," alisema Joyce.

OCHA ilisema kuwa watu 123 katika vifo hivyo vilikuwa vya wafanyakazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA) ambavyo vilitokana na mashambulizi ya anga ya jeshi la Israel.

Ofisi hiyo ya Umoja wa Mataifa ilisema kwamba mwaka huu huenda ukawa mbaya zaidi, kwani kufikia Agosti 7, tayari wafanyakazi 172 walishauawa.

Taarifa iliyotolewa na OCHA ilizugumzia pia jinsi hali inayozidi kuwa mbaya nchini Sudan na Sudan Kusini ilivyochangia ongezeko hilo la idadi ya wafanyakazi wa huduma za kibinaadamu wanaouawa wakiwa kwenye kazi zao.

Ilielezwa kuwa mashirika ya kibinaadamu kote ulimwenguni yaliyoandikia barua mataifa wanachama wa Umoja wa Mataifa kuyataka yachukuwe juhudi zaidi za kuwalinda wafanyakazi wa misaada.

"Tutaendelea kubakia na kuhudumia kwenye maeneo yenye migogoro kote duniani, lakini hali inatutaka tuwe na msimamo wa pamoja na kutoa wito wa kulindwa wafanyakazi wetu, wahudumu wa kujitolea na raia tunaowahudumia," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mbali na Palestina, Sudan na Sudan Kusini, mataifa mengine yaliyomo kwenye orodha ya nchi 10 zenye mauaji mengi zaidi ya wafanyakazi wa misaada ni pamoja na Israel na Syria, ambako wafanyakazi saba waliuawa kwa kila nchi.

Vile vile, ilielezwa kuwa Ethiopia na Ukraine, wafanyakazi sita waliuawa kwa kila nchi, Somalia watano, na vifo vinne kwa kila moja kati ya Myanmar na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). **DW**

HABARI MICHEZO

# AUSSEMS: UWANJA UMEIOKOA KENGOLD KULA MABAO MENGI

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA Mkuu wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, amesema timu yake ingeweza kufunga idadi kubwa ya mabao dhidi ya KenGold kama Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ungekuwa kwenye hali nzuri.

Mbelgiji huyo alisema hayo, baada ya kukamilika kwa mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara, timu yake ikiichakaza KenGold na kuondoka na ushindi wa mabao 3-1.

Aussems, alisema KenGold inabidi waushukuru uwanja kwani umewasaidia kupunguza mabao, kwa sababu uliwafanya wasicheze kwenye kiwango chao cha kawaida.

"Tulijitahidi kucheza vizuri, lakini uwanja haukuwa rafiki, tulicheza kwenye mazingira magumu, hatukucheza kwenye kiwango chetu, lakini tunachoshukuru ni kwamba tumepata ushindi, ambao ni mzuri hasa katika mchezo huu wa kwanza wa Ligi Kuu," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Aussems alisema kwa kuthibitisha hilo mashabiki wataona mechi ijayo ambayo wanakwenda kucheza dhidi ya Kagera Sugar, Uwanja wa Kaitaba uliopo mjini Bukoba, ambao unaruhusu kucheza soka la chini na pasi nyingi.

"Tunakwenda Kagera, huko mtaona kitu tofauti na hiki, najua kule kuna uwanja mzuri, tutacheza soka safi zaidi ya mchezo huu," alisema kocha huyo.

Ilikuwa ni siku mbaya kwa KenGold ambayo ni mechi yake ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara kihistoria tangu kuanzishwa kwake, kwani ilikutana na dhahama ya kuchapwa mabao 3-1 mbele ya mashabiki wake.

Timu hiyo imepanda daraja msimu huu ikitokea Ligi ya Championship.


Magoli ya Singida Black Stars yalifungwa na Emmanuel Kayekeh dakika ya 41, Elvis Rupia (dk ya 62) na Mohamed Damaro (dk ya 81), huku bao la kufutia machozi kwa KenGold likifungwa na Joshua Ibrahim, dakika ya 68.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fikiri Elias, alielezea mambo kadhaa yaliyosababisha timu yake kupoteza ambayo ni kutokuwa na uzoefu, udhaifu kwenye safu yake ya ulinzi na pia alionekana kutoridhishwa sana na uamuzi.

"Mchezo ulikuwa mgumu, sitaki kusema mengine, tulikuwa tunaona kuna changamoto katika kuuendesha mchezo wenyewe pande zote tatu yaani sisi, wapinzani wetu, lakini pia hata waliopewa dhamana ya kuusimamia mchezo wenyewe, tuliona hawakuwa sawa, ila hatuwezi kulalamika sana.

"Nirudi kwetu wenyewe, uzoefu umetuangusha, tumefungwa mabao yanayofanana, nadhani tuendelea kuwafundisha vijana wetu wawe na nidhamu ya ulinzi," alisema.

HESABU...



Beki wa kulia wa Yanga, Yao Kouassi, akipiga hesabu ya kumhadaa mchezaji wa Vital'O ya Rwanda kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex Jumamosi iliyopita na Yanga kushinda mabao 4-0. Timu hizo zitarudiana mechi ya mkondo wa pili Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA yatoa milioni 40/- Ndondo Cup

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetangaza kudhamini Mashindano ya Ndondo Cup, kwa kutoa Sh. milioni 40.5 kwa kushirikiana na Uongozi wa Michezo wa Shadaka.

Udhamini huo unatokana na dhamira ya TRA ya kukuza ushirikishwaji wa jamii kupitia michezo huku ikikuza mipango muhimu ya elimu ya kodi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema udhamini huo unaosimamiwa na Kampuni ya Shadaka Sports Management, utasaidia michuano ya Ndondo Cup inayoendelea ambayo ni miongoni mwa mashindano maarufu ya soka nchini.

"Kama sehemu ya ushirikiano huu, TRA itatumia jukwaa la Ndondo Cup kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu Stempu zake za Kielektroniki za Ushuru (ETS) na Kampeni ya Hakiki Stampu. Ujumbe muhimu wa udhamini huu ni kuangazia umuhimu wa kuhakiki bidhaa kabla ya kuzitumia ili kuhakikisha kuwa ni salama, ni halisi na zinatii kanuni za kodi," alisema na kuongeza kuwa;

"Ushirikiano huo na Ndondo Cup ni fursa ya kipekee kwa TRA kuwasiliana na wananchi kwa njia sahihi. Kupitia michezo, tunaweza kufikia hadhira kubwa zaidi ili kuwaelimisha na kuwashawishi kufahamu suluhisho la kisasa zaidi la Stempu za Ushuru za Kielektroniki katika kuhakikisha uhalisi wa bidhaa. Zaidi ya hayo, tunaamini kuwa kupitia mpango huu, tunaweza kuleta mabadiliko makubwa kwa tabia za watumiaji na kuchangia katika lengo pana la kuimarisha uzingatiaji wa kodi kote nchini," alisema

Aliongeza kuwa TRA inatoa wito kwa watumiaji wa bidhaa zenye Stempu za Ushuru za Kielektroniki (ETS) kupakua programu ya Uthibitishaji wa Stempu na kuhakiki bidhaa hizo kabla ya kuzitumia kwani hiyo ni njia mojawapo ya kulinda afya zao na kuhakikisha serikali inapata mapato sahihi ya kodi.

Mkurugenzi Mkuu wa Usimamizi wa Michezo wa Shadaka, Shaffih Dauda, aliishukuru TRA, huku akisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kampuni katika kuongeza thamani ya michezo ya ndani.

"Tunafuraha kuwa na TRA kama wadhamini wakuu wa Ndondo Cup mwaka huu. Udhamini huu si tu kwamba unasaidia maendeleo ya soka nchini, lakini pia una lengo kubwa zaidi kwa kuelimisha umma juu ya masuala muhimu ya kodi, vilevile viwanja vyetu vya michezo vinajaa bidhaa mbalimbali, hivyo tunatarajia ushirikiano huu ili kuhakikisha teknolojia hii inasaidia kujikinga na bidhaa feki tunapokuwa viwanjani," alisema Dauda

# 10 kuiwakilisha Tanzania Chess nchini Hungary

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Kimataifa ya Olympiad ya mchezo wa Chess 2024, yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi ifikapo Septemba 10 hadi 23, mwaka huu huko Budapest nchini Hungary, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni Msemaji wa Chama cha Mchezo wa Chess Tanzania (TCA), Musa Manula, alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi 192 kutoka mataifa mbalimbali, ambapo Tanzania itawakilishwa na timu mbili ya wanaume na wanawake.

Alisema timu hizo zinaundwa na wachezaji kumi ambapo kati yao wasichana wapo watano na wanaume watano.

"Hizi timu zinaundwa na wachezaji kumi ambao walifanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali walioshiriki, hivyo tunaamini watakwenda kuiwakilisha vema nchi yetu," alisema Mangula.

Aidha, aliipongeza Kampuni ya Bankable ambayo ndio wadhamini wao wakuu kwa kukubali kugharamia safari nzima pindi timu hizo zitakapoanza safari yao kuelekea nchini Hungary.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Bankable ambao ndio wadhamini wakuu, Ivan Tarimo, alisema wameamua kutoa udhamini kwa lengo la kuukuza zaidi mchezo huo.

"Tumeamua kutoa udhamini kwa Chama hiki baada ya kugundua kuwa Chess ni mchezo ambao unapendwa kuchezwa na watu wengi, vilevile kuuinua zaidi ili ufike mbali kama ilivyokuwa michezo mingine," alisema Tarimo.

# Serikali yakunwa viwango Tenisi

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imeeleza kufurahishwa na viwango vilivyooneshwa na vijana wenye umri chini ya miaka 12 katika Mashindano ya Mchezo wa Tenisi Afrika Mashariki yaliyomalizika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Klabu ya Gymkhana, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kufunga mashindano hayo Jumamosi iliyopita, Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, alisema kwa viwango hivyo anaamini miaka ijayo watapatikana wachezaji wazuri wa timu ya taifa.

"Nimefurahishwa na viwango vilivyooneshwa na vijana katika mashindano haya, naamini miaka ijayo tutakuwa na timu nzuri ya taifa," alisema Mayay.

Alisema licha ya timu ya Tanzania kutotwaa kombe la mashindano hayo, wataendelea kushirikiana na viongozi wa chama hicho kuhakikisha mchezo huo unazidi kukua.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TONEY ATAKIWA SAUDIA
WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, wako kwenye mazungumzo na Klabu ya Saudi Arabia, Al-Ahli ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. (***Teamtalks***)

### PEP MKATABA MPYA
KLABU ya Manchester City inataka kocha Pep Guardiola mwenye umri wa miaka 53, kuamua iwapo atasaini mkataba mpya na klabu hiyo kabla ya Krismasi. Mkataba wa sasa wa Mhispania huyo utaendelea hadi 2025. (***Sky Sports)***

### MORENO AGOMBEWA
KLABU za Nottingham Forest, Villarreal, Sevilla, na Valencia zinataka kumnunua beki wa Aston Villa na Hispania, Alex Moreno mwenye umri wa miaka 31. (***Football Insider)***

### PELLISTRI AJADILIWA
KLABU ya Panathinaikos iko kwenye mazungumzo na Manchester United kuhusu mkataba wa kiungo wa kati wa Uruguay, Facundo Pellistri, 22. (***Athletic)***

### GUERRA NA ATLETICO
ATLETICO Madrid haijapuuza uhamisho wa kiungo wa kati wa Valencia na Hispania, Javi Guerra mwenye umri wa miaka 21, huku mkataba wao wa kiungo wa kati wa Chelsea na Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, ukikwama. (***Mail***)

### LIVERPOOL KUSUBIRI
LIVERPOOL itasubiri hadi dirisha la usajili la Januari kumsajili kiungo nyota baada ya hatua ya klabu hiyo kumnunua Mhispania Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25 kutoka Real Sociedad kushindikana. (***Football Insider)***

### MCTOMINAY ATAKIWA
KLABU ya Fulham imeanzisha tena mazungumzo na Manchester United kuhusu usajili wa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay, 27. (***Sky Sports***)


### NAPOLI NAO WAJITOSA
MKURUGENZI wa michezo wa Napoli, Giovanni Manna amekataa kufuta mpango wa kumnunua Scott McTominay. (***Manchester Evening News***)

### VINICIUS SASA ASAKWA
KLABU ya Las Palmas imewasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Fulham raia wa Brazil, Carlos Vinicius mwenye umri wa miaka 29, ambaye pia anasakwa na Corinthians. (***Sky Sports***)

### LACROIX SAFI PALACE
KLABU ya Crystal Palace imefanikiwa katika mpangi wa kumsaka beki Mfaransa, Maxence Lacroix mwenye umri wa miaka 24 kutoka Wolfsburg. (***Sky Germany)***.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND KIWANGO NI KAMA MESSI, RONALDO – GUARDIOLA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema rekodi ya Erling Haaland ya kufunga mabao inafikia viwango vya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, lakini anaamini kuwa mshambuliaji huyo anaweza kuwa bora zaidi katika miaka ijayo.

**Haaland mwenye umri wa miaka 24, alifunga bao la kwanza dakika ya 18 wakati City ikianza haraka ti zake za kusaka taji la tano mfululizo la Ligi Kuu England.**

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Norway alifunga mechi yake ya 100 kwenye ligi kwa kufunga bao lake la 91, na Guardiola alidai kuwa majira ya joto ya Haaland - Norway ilishindwa kufuzu kwa Euro 2024 - hivyo kumemfanya ajihisi mkali zaidi kabla ya kampeni mpya.

"Ana namba za Messi na Cristiano Ronaldo, ambao walidhibiti muongo uliopita, miaka 15, kila kitu," alisema Guardiola.

"Katika suala la namba, ni kiwango hicho. Kwa hiyo, sijui anafanyaje,

**●●● Ana namba zao, michezo 100 kufunga mabao 91 ni jambo la kushangaza katika...**

lakini katika michezo 100 kufunga mabao 91 ni jambo la kushangaza katika Ligi Kuu ya nchi hii.

"Nilikuwa na hisia kwamba anajisikia vizuri zaidi kuliko msimu uliopita katika hatua hii. Baada ya kusafiri msimu uliopita, alijisikia hivyo-hivyo au alihisi amechoka. Msimu huu, nadhani kwa Euro kwa bahati mbaya Norway haikuwapo, kulikuwa na kupumzika zaidi na ndio, anahisi vizuri.

"Bao lilikuwa zuri sana. Mchango wake katika mambo mengi. Alikuwa na nafasi mbili au tatu na kila mara nilikuwa na hisia kwamba kuna pengo la kuboresha kama mchezaji wa soka."

City wanaweza kukabiliwa na msimu wa michezo 75 ikiwa watatinga fainali ya kila mashindano, pamoja na Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia huko Marekani msimu ujao wa kiangazi, na Guardiola alikiri kwamba anaweza kushawishiwa kuwapa wachezaji mapumziko binafsi wakati wa msimu kama ilivyopendekezwa na kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti.

"Labda, na kama Carlo atasema, labda nisikilize na nitamfuata," alisema Guardiola

"Labda katika muda fulani, wanacheza sana, sana, nenda wiki moja nyumbani, usiwe kwenye mazoezi na urudi. Ndio maana katika maandalizi ya msimu mpya, baada ya kushinda kile tulichoshinda, michezo mingi, kuburudisha kama umechoka hapa kichwani mwako, sahau kuhusu hilo, huwezi kustahimili.

"Lazima kuwe na nia ya kuwa hapa, bado kufurahia kucheza mpira, kufurahia vipindi vya mazoezi, kuwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo pamoja. Hii inapotokea, unaweza kudai kila kitu.



# ANCELOTTI AKOSOA KIWANGO CHA MADRID

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alikosoa 'mtazamo' Pamoja na 'kujitolea' kwa timu yake ya Real Madrid baada ya mabingwa hao wa LaLiga kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mallorca katika mchezo wao wa ufunguzi wa msimu wa 2024-25.

Rodrygo aliiweka Madrid mbele katika dakika ya 13 kwenye Uwanja wa Son Moix - baada ya pasi iliyowahusisha Kylian Mbappe, Jude Bellingham na Vinicius Junior - kabla ya Vedat Muriqi kuisawazishia Mallorca kwa kichwa kipindi cha pili.

Madrid haikuweza kupata bao la ushindi dakika za lala salama, na beki Ferland Mendy alitolewa kwa kadi nyekundu katika muda ulioongezwa, na kumwacha kocha Ancelotti akiwa amechanganyikiwa.

"Katika kipindi cha pili tulikosa usawa," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

„Tulitoa mashambulizi ya kupingana, krosi. Haukuwa mchezo mzuri. Tunapaswa kulinda vema, na zaidi ya yote tuwe na usawa zaidi uwanjani.

"Leo hatuna furaha. Sitaki kutoa visingizio. Ilibidi tu kufanya vizuri, kwa mtazamo zaidi. Lakini tunaweza kujifunza mengi kutoka kwa mchezo huu, ilikuwa wazi ni wapi tulikuwa na matatizo."

Madrid walishinda LaLiga msimu uliopita, wakimaliza kwa pointi 10 mbele ya wapinzani wao wa karibu Barcelona, na wamemuongeza mshambuliaji Mbappe kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint-Germain.

Mbappe alicheza dakika zote 90 dhidi ya Mallorca na akapiga mashuti manne, mawili yakilenga lango.

Ancelotti aliisifu Mallorca, inayofundishwa na kocha mpya Jagoba Arrasate, akitaja droo hiyo kuwa „matokeo sahihi."

"Ulinzi haukuwa mzuri, ilikuwa ngumu kwetu kushinda mpira baada ya kuupoteza," alisema Ancelotti.

# Slot asema Salah ana miaka mingi Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot anaamini Mohamed Salah bado ana miaka mingi iliyosalia kwenye kiwango cha juu baada ya kufunga bao katika ushindi wao wa mabao 2-0 dhidi ya Ipswich Town Jumamosi iliyopita.

'Wekundu' hao walianza msimu wa 2024/25, wa kwanza kwa Slot kwenye usukani tangu kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp, kwa ushindi katika mchezo wa mapema Jumamosi kwenye Uwanja wa Portman Road.

Diogo Jota alitikisa nyavu kabla ya Salah kuibuka na bao la pili na la ushindi dakika za lala salama.

Bao hilo lilimaanisha kwamba, Salah sasa amesajili mabao 300 ya kuvutia katika mechi 350 alizocheza Liverpool.

Akiwa na umri wa miaka 32, itakuwa rahisi kudhani kwamba Salah angepungua, lakini Slot alifichua baada ya mechi kuwa, amefurahishwa na jinsi Mmisri huyo anavyojiendesha.

"Nikiona anachofanya kuweka mwili wake kama ni kuwa tayari kucheza kila mchezo, basi nadhani kuna miaka mingi zaidi ndani yake ya kucheza," alisema Slot kuhusu Salah.

"Lakini sasa naitazama Brentford Jumapili ijayo na si mwisho wa msimu, siamini watu binafsi, naamini zaidi katika timu. Mo anaweza kufunga mabao kwa sababu ya kukimbia vizuri kutoka kwa wachezaji wengine, au kwa sababu ya timu zilizojengeka kwa hiyo nadhani Mo pia anahitaji timu."

Salah amebakiza mwaka mmoja tu kumaliza mkataba wake, kama ilivyo kwa nahodha Virgil van Dijk na makamu nahodha Trent Alexander-Arnold.

Watatu hao wataruhusiwa kuzungumza na klabu nyingine Januari Mosi, mwakani na kuendelea ikiwa hawajaafikiana mikataba mipya kufikia wakati huo.



## Maresca atetea uamuzi wa kumpa unahodha Fernandez

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Enzo Maresca, ametetea uamuzi wake wa kumchagua Enzo Fernandez kama nahodha mwezi mmoja tu baada ya kiungo huyo wa Argentina kutuma video yenye wimbo unaodaiwa kuwa wa kibaguzi.

Fernandez alivaa kitambaa hicho Chelsea ilipochapwa mabao 2-0 na Manchester City katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 - ambaye pia alipiga goti kabla ya mechi kuanza kama sehemu ya timu zote zinazoshiriki kampeni inayoendelea ya Ligi Kuu England ya kupinga ubaguzi - alilazimika kuomba msamaha baada ya kupakia video ambayo alikejeli baadhi ya wachezaji wa Ufaransa.

Mchezaji mwenzake wa Chelsea, Wesley Fofana aliitaja video hiyo kuwa ni ya „ubaguzi wa rangi usiozuiliwa" wakati huo, lakini akasisitiza kwamba Fernandez hakuwa mbaguzi wa rangi na alikubali msamaha wake.

Fernandez alikuwa nahodha wa timu hiyo wakati nahodha wa Reece James akikosekana na Maresca alisema: „Enzo ni mmoja wa manahodha wa timu hii, si yeye pekee. Tuna Reece James, tuna baadhi ya manahodha wa timu hii.

"Sababu ni kuwaona wachezaji wenzake wanamtambua, kama nahodha, na tayari alikuwa nahodha katika maandalizi ya msimu tulipombadilisha Reece kwenye mchezo.

"Sote tunafanya makosa. Ni muhimu kutambua Enzo alifanya kosa, akatambua kosa na imekamilika.

"Sijui wewe ila nilifanya makosa huko nyuma nikayatambua, kama binadamu ukikosea ukalitambua hutaadhibiwa maisha, Enzo alikosea. kutambuliwa kwangu, yeye ni mmoja wa marejeleo na sina cha kuongeza."



# KOCHA AZAM AANIKA SABABU KUPATA USHINDI MWEMBAMBA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema hawakupata ushindi mkubwa nyumbani kwa sababu wachezaji wake walionekana kucheza kwa presha ya kutaka kufunga mabao mapema na walipokuwa wanashindwa kufanya hivyo walikuwa wanatoka mchezoni na kushindwa kufuata maelekezo yake.

Raia huyo wa Senegal, alisema hayo baada ya timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya APR ya Rwanda kwenye mchezo wa hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es salaam juzi.

Pamoja na ushindi huo kiduchu, kocha huyo alisema ana matumaini ya timu yake kusonga mbele na kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

"Nafikiri wachezaji walikuwa na hofu, kama walikuwa wanataka kufunga mabao ya haraka haraka dakika za mwanzo, lakini kila muda ulivyozidi kwenda hawapati, walikuwa wakiingiwa na presha na kushindwa kucheza kwa maelekezo.

Mapumziko niliwaambia wasiwe na haraka kwa sababu hii ni mechi ya kwanza, ya marudiano tutacheza Rwanda, hivyo watulie, watapata nafasi watafunga na hata wasipofanya hivyo leo (juzi), hata mechi ya mkondo wa pili wanaweza kufunga pia," alisema Dabo.


Azam ilipata ushindi huo kwa bao lililofungwa na straika raia wa Colombia, Jhonier Blanco dakika ya 56 kwa mkwaju wa penalti, baada ya Feisal Salum kuangushwa ndani ya eneo la hatari.

"Nimeifutilia APR ni timu ambayo huwa hairuhusu mabao kirahisi, mabeki wake wapo vizuri, kwa maana hiyo inabidi tujipange vema katika mechi ya marudiano.

„Tunakwenda kucheza nchini Rwanda, tuna uhakika wa kushinda kwa sababu tuna kikosi kizuri cha kuweza kushinda pia ugenini," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa APR, Mserbia Darko Novic, alisema ana wasiwasi kama ilikuwa penalti sahihi, lakini akawapongeza wachezaji wake kwa kufanikiwa kuwazuia Azam.

"Tumecheza na timu nzuri, tumepoteza kwa bao 1-0, kwa hiyo tunajipanga kwa mchezo ujao, ila kuna nafasi tumepoteza ambazo zingeweza kufanya mchezo uishe kwa sare," alisema Darko.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro (kushoto), akimkabidhi mchezaji wa Azam FC, Adolf Mutasingwa, kitita cha Sh. milioni tano kwa niaba ya Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameahidi kutoa Sh. milioni tano kwa kila bao la ushindi litakalofungwa na klabu za Tanzania zinazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa. Azam ilishinda bao 1-0 dhidi ya APR ya Rwanda kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Fadlu aiona Simba ikiwa tishio Afrika

INATOKA UK. 24

Yalikuwa ni mabao ya beki wa kati, Fondoh Che Malone, Valentine Mashaka na Awesu Awesu, yaliyofanya Simba kupata ushindi wa mabao 3-0, yaliyoipeleka kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Francis Kimanzi, Kocha Mkuu wa Tabora United, alisema hawezi kuwalaumu wachezaji wake kwa sababu wamekutana na mechi kubwa na ngumu, dhidi ya timu imara

"Nafikiri wapinzani wetu walikuwa bora, wamefanya kile walichotaka kufanya, wana vitendea kazi bora kuliko sisi kwa maana ya wachezaji, sitaki kuwaangusha wachezaji wangu kwa sababu wamefanya vema, wamefanya kila walichokiweza, ndiyo maana siko hapa kuzungumzia jinsi tulivyofungwa, tunatengeneza timu taratibu baadaye tutakuwa timu bora," alisema raia huyo wa Kenya.

Wakati Tabora United itakwenda mkoani Lindi kucheza dhidi ya Namungo, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Jumapili ijayo, siku hiyo hiyo, Simba itakuwa nyumbani, Uwanja wa KMC, Mwenge, ikiikaribisha, Fountain Gate.



## Gamondi ataka Yanga kufuzu kwa rekodi CAF

INATOKA UK. 24

kupata idadi hiyo ya mabao, na inawezekana yangekuwa mengi zaidi kama isingekuwa hivyo, Jumamosi Uwanja wa Mkapa, mambo yatakuwa tofauti, mashabiki wa Yanga watafurahi zaidi," alisema.

Yanga ilipata mabao yake kupitia kwa Prince Dube, Clatous Chama, Clement Mzize na Stephane Aziz Ki.

Wakati Gamondi akinena hayo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amewataka wanachama na mashabiki wa Yanga kumiminika kwa wingi Jumamosi ijayo, saa 1:00 usiku katika mechi hiyo ya mkondo wa pili huku akitangaza viingilio vya mechi hiyo kuwa ni Sh. 30,000 kwa VIP A, Sh. 20,000 VIP B, Sh. 10,000 VIP C na Sh. 5000 kwa viti vya mzunguko 5000.

Alisema ushindi mnono walioupata Jumamosi iliyopita, utawafanya mashabiki wa timu hiyo kwenda uwanjani kama mtoko wa kifamilia, kwani hawatokaa kwa wasiwasi, badala yake watakuwa wanafurahia soka.

"Hatutakaa uwanjani kwa presha, mashabiki watakuwa wakiangalia mpira huku wakila na kunywa kwa furaha, huku wakifurahia soka, kwa hiyo sidhani kama ni mechi ya kukosa," alisema Kamwe.



# Simba yamburuza Mnunka TFF kwa utoro

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema inaandaa barua kwa ajili ya kuiwasilisha Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kumshtaki straika wa timu yao ya wanawake, Simba Queens, Aisha Mnunka, kutokana na utovu wa nidhamu aliouonesha wa kutoonekana kambini, kabla ya kutoa taarifa rasmi kwa wanachama na mashabiki.

Akizungumza akiwa nchini Ethiopia ambako wanashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Kanda ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Mratibu wa timu hiyo, Selemani Makanya, aliema mpaka jana ambako ilitarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya FAD ya Djibouti, hawana taarifa ya mchezaji huyo ambaye alitakiwa awepo kwa ajili ya kuitumikia timu hiyo.

Makanya, alisema mara ya mwisho mchezaji huyo alikuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa, Twiga Stars, lakini baada ya kuvunja kambi, hakurejea kikosi cha Simba Queens ambacho kilikuwa kinajiandaa na michuano hiyo.


"Mnunka bado ni mchezaji wetu, ana mkataba wa mwaka mmoja, alikwenda timu ya taifa, alitakiwa ajiunge na kambi yetu, hakuja na hakutoa udhuru wowote kama ana matatizo au anaumwa, ameamua tu kukaa kimya, sisi kama viongozi tumetumia jitihada kubwa kumtafuta tumeshindwa, simu yake haipatikani na taarifa zinasema amebadilisha namba za simu," alisema mratibu huyo.

Taarifa zinadai kinara huyo wa mabao kwenye Ligi Kuu ya Wanawake msimu uliopita, yupo jijini Dar es Salaam na amefichwa na timu moja mpya jijini humo, kitu ambacho kimewakasirisha viongozi wa timu hiyo na kuamua kuwaandikia barua TFF.

Taarifa inaeleza katika barua hiyo, viongozi pia wataitaja timu ambayo inamrubuni mchezaji wao wakati inajua haiwezi kumtumia kwani bado ana mkataba wa mwaka mmoja na Simba Queens.


"Kinachofuata uongozi wa Simba umeandaa barua ya kuitaarifu TFF juu ya utovu wa nidhamu wa mchezaji huyo, na baadaye klabu itatoa taarifa rasmi kwa wanachama na mashabiki wa Simba ili kupunguza sintofahamu na maswali mengi juu ya hili lililotokea," alisema.

Michezo
Nipashe
Jumanne Agosti 20, 2024



Ancelotti akosoa kiwango cha Madrid UKURASA 22

HEKAHEKA...



Beki wa kati wa Simba, Che Fondoh Malone, akiruka sambamba na mshambuliaji Steven Mukwala katika harakati za kuwania kuifungia timu yao kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tabora United iliyopigwa juzi katika Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam. Katika harakati hizo, Che Malone ndiye aliyeuwahi mpira na kuiandikia timu yake bao la kwanza kwa kichwa wakati ikishinda 3-0 kwenye mchezo huo. **MPIGAPICHA WETU**

## Fadlu aiona Simba ikiwa tishio Afrika

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaambia wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa wawe na subira kidogo, kwani kikosi chake kinaelekea kwenye ubora anaouhitaji, na ana uhakika itakuwa ni tishio zaidi si hapa nchini tu bali Afrika.

Raia huyo wa Afrika Kusini alitoa kauli hiyo juzi, baada ya kumalizika kwa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Tabora Uited, ikishinda mabao 3-0, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema bado anaendelea na kazi yake ya kukiimarisha kikosi hicho, lakini akiridhika na jinsi walivyocheza na kupata ushindi huo.

"Timu inaanza kuimarika, siku hadi siku inaelekea kwenye ubora ninaotarajia, mashabiki wa Simba wawe na subira kwa sababu bado tunaendelea kukiweka kikosi kwenye hali nzuri, na kukifanya kiwe bora zaidi na tishio.

Bado tuna shughuli ya kufanya, ukiangalia katika mechi hii ilikuwa tuiue mapema tu kipindi cha kwanza na kipindi cha pili tucheze bila presha kwa kuudhibiti na kuumiliki mchezo, lakini haikuwa hivyo, tukalazimika kusaka mabao ya kuumaliza mchezo kipindi cha pili, lakini nimeridhika, ila nimehuzunika kuumia kwa Mutale (Joshua), kidogo kidogo tunakwenda," alisema Fadlu ambaye ndiyo msimu wake wa kwanza kuifundisha timu hiyo akitokea, Raja Casablanca ya Morocco.

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi ataka Yanga kufuzu kwa rekodi CAF

●●● Asema kwa Mkapa Vital'O itakutana na gharika zaidi ya mabao Jumamosi, kuziona buku tano...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupata ushindi mnono wa mabao 4-0 Jumamosi iliyopita dhidi ya Vital'O ya Burundi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema wanahitaji ushindi mwingine mkubwa katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali, Jumamosi ijayo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Gamondi, alisema katika mchezo huo hawataenda kuzuia, au kulinda ushindi walioupata Jumamosi iliyopita, bali wanahitaji ushindi kwa mara nyingine tena na anadhani utakuwa mkubwa zaidi, kwa kuwa wanakwenda kucheza katika uwanja ambao watakuwa huru zaidi na mpira.

**"Tunataka kushinda tena kwenye mchezo wa marudiano, wala hatuendi kuzuia, au kulinda ushindi wetu uliopita. Jumamosi ijayo tunacheza kama tulivyocheza mechi iliyopita, tunataka kufuzu, lakini tunataka kufuzu kwa kishindo," alitamba Gamondi, raia wa Argentina.**

Alisema anamaanisha anachokiongea kwa sababu ana wachezaji bora wenye uwezo wa kuifanya kazi hiyo, ana kikosi kipana kwa sasa ambacho mchezaji anayeingia anakwenda kufanya kama kile kilichofanywa na aliyetoka au zaidi.

Gamondi alisema ana uhakika wa ushindi mkubwa zaidi kutokana na kwenda kucheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambao ni mkubwa zaidi ya ule wa Azam Complex, utakaowafanya wachezaji wake wawe huru zaidi kutokana na aina ya mpira wanaocheza.

"Najua tunakwenda kucheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, tutacheza vizuri zaidi tofauti na ilivyokuwa Azam Complex, kwa sababu ni mkubwa zaidi na kutakuwa huru zaidi kwa aina yetu ya uchezaji mifumo yetu pia, ndiyo maana nasema tunaweza kupata ushindi mkubwa zaidi na kucheza soka safi zaidi ya mchezo uliopita.

Vital'O, iliutumia Uwanja wa Azam Complex hapa nchini, kama uwanja wao wa nyumbani, kutokana na kutokuwa na viwanja vilivyopitishwa katika michezo ya kimataifa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Gamondi pia alielezea hali ya hewa iliyochangia wachezaji wake kutopata mabao mengi zaidi katika mchezo uliopita.

"Katika mechi iliyopita tuliathiriwa zaidi upepo, wachezaji wangu walinilalamikia kuhusu hilo, kwa hiyo walishindwa kufanya kwa usahihi baadhi ya mambo ikiwamo kupiga pasi sahihi, nadhani hilo pia lilichangia

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >